

Maji Yaliyopo Daima Yatokayo Mwambani

Jeffersonville, Indiana, USA

Julai 23, 1961A

1 Tunashukuru asubuhi ya leo kwa ajili ya Uwepo wa Bwana Mungu, ambao ungeanzisha ibada za mwanzoni kwa kutupa ujumbe, kwamba—kwamba tunapaswa “kusikiliza, kuwa na kicho” mbele Zake, ya kwamba Yeye ana jambo la kutuambia. Nina hakika ya kwamba Yeye atafanya yale aliyoahidi. Yeye daima hutimiza Neno Lake. Na kwa hiyo tunashukuru kukusanyika pamoja, tukiwa hai, na upande huu wa umilele asubuhi ya leo, na kuweza kumwabudu Bwana tena, na kukusanyika pamoja na kusikia kutoka Kwake. Hiyo ndiyo sababu tunakutana, ni kwa kusudi hili hasa.

2 Sasa, kwa namna fulani nilimvamia Ndugu Neville, bila kutarajiwa, leo hii, kwa sababu ya ndoto fulani niliyopata. Ambayo ... Ninaamini katika—katika ndoto. Ninaamini ya kwamba Mungu hushughulika na watu kwa ndoto. Nami nilipata ndoto isiyo ya kawaida sana, juzi usiku, kwamba, nilikuwa nikipita ubavuni mwa kilima, ubavuni mwa kilima fulani, nikienda kwenye mkahawa fulani ambapo nilikuwa nile chakula cha—changu cha jioni. Nami niliona ya kwamba, nilipokaribia mahali hapo, walikuwa wakipiga muziki, okestra ilikuwa ikipiga muziki kwa fidla, na kuwaburudisha watu walipokuwa wakila. Na kulikuwako na jambo fulani kuuhusu ambalo halikunipendeza, kwa hiyo nikapita tu kitu hicho. Ndipo nikakutana na mtu mmoja akikwea kilima. Nami nikaangalia, na watu wengi walikuwa wakikwea kilima hicho wakielekea kwenye mkahawa huu. Lakini kwa namna fulani niliwaondokea, nikageuka upande wa kulia, ama, wa kushoto.

3 Na kwa namna fulani, huko chini bondeni, ningeweza kuona maskani. Nikaisikia sauti ya mtu fulani, ikasema, “Mlaki Ndugu Branham kwenye njia panda fulani-fulani. Yeye anashuka chini ya kilima kule juu. Na umwambie jambo fulani-fulani.” Ndipo nikafanya hima kufika kwenye hiyo njia panda.

Ndipo wakati mtu huyo alipokuja, ilikuwa ni Ndugu Neville amevaa suti yake ya hudhurungi, alionekana kama tu vile anavyoonekana ameketi pale asubuhi ya leo. Ndipo akasema, “Ndugu Branham, kama utakuwako humu mjini,” kasema, “lingekuwa ni jambo zu—zuri kwako kushuka uje, kwa maana Ndugu Hank...” Sasa, yule pekee nimjuaye, Ndugu Hank, ni Ndugu Henry Carlson, tunamwita Hank. Kasema, “Huenda akawazia lilikuwa ni jambo lisilo kawaida kwamba hukuitembelea maskani zaidi kama utakuwako huku mjini, ama humu jijini kwa siku chache.” Nikaamka.

Na, kwa jambo hilo, kwa namna fulani nilijisikia visivyo kawaida. Sikutaka kuvamia katika wakati huo wa juma, mpaka nilipomuuliza Ndugu Neville iwapo alikuwa na jambo lolote maalum kwa ajili ya asubuhi hii, kwa ajili ya kanisa. Kwa hiyo alikuwa na fadhili, kama kawaida, kasema, “Njoo huku chini.” Kwa hiyo, tumekuja tu. Nilimpigia simu jana jioni na nikaja asubuhi hii bila kutarajiwa na yeyote kwetu.

4 Sasa ninaamini ya kwamba lingekuwa ni jambo jema, kwanza, kwangu mimi kwa namna fulani ku—kuwaelezeni mambo fulani. Mimi, ninadhaniwa, ni mtu wa kipekee sana kwa watu wengi. Nami kwa namna fulani ni wa kipekee kwangu mimi mwenyewe, pia. Kwa sababu ninajaribu kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu kwa karibu niwezavyo. Na hilo linatufanya wa kipekee. Mnaona? Tunafanya mambo ambayo kweli tu—tunaketi chini na kushangaa wakati mwingine, “Ni kwa nini nikafanya jambo kama hilo? Nilipataje kamwe kufanya jambo kama hilo?” Na papo hapo huenda ukafikiri ya kwamba umefanya yale hasa usiyopaswa kufanya. Lakini kama tu utakuwa mvumilivu, na uwe na imani, nawe una hakika ya kwamba Mungu amekuongoza kufanya jambo hilo, utaona ya kwamba linafanya kazi vizuri kabisa. Mnaona? Na mara nyingi tunaona jambo hilo. Nami ninajua Ndugu Neville amepata hilo mara nyingi. Na viongozi na watu wa kiroho wanatambua jambo hilo.

Imekuwa wakati mwingine maishani mwangu kwamba... Kusema kweli, tangu nilipokuwa tu mvulana, kamwe sijasikia kuongozwa hasa kwamba inanipasa kuishi Je—Jeffersonville. Daima imekuwa ni kero, kwangu kujaribu kuishi hapa. Kwanza, hali ya hewa haikubaliani nami. Jambo lingine, inaonekana kuna kukandamizwa kwa roho.

5 Ukirejea nyuma na kuangalia mahali fulani hapa, kama haikuharibiwa katika wakati ule wa mafuriko, kuna barua kuhusu hilo, niliyokuwa nayo, nilipoitwa hudumani kwa mara ya kwanza, nilianza kuondoka. Na mimi na Ndugu George DeArk ...

Na mama yake Ndugu Graham Snelling, Ndugu Hawkins ambaye anaendesha kituo cha petroli huko New Albany, na watu wengine wengi, walikutana nami nje ya mahali padogo pa mkutano wa maombi huku, na hata wakasema, kama ningekaa, wangewapunguzia watoto wao chakula mezani, ku—kuijenga maskani, kusudi isivalazimu kuchukuliwa mahali mahali.

6 Nilipomsikia maskini mama huyo, akiwa amemshika mtoto mmoja kwa mkono wake na huyo mwingine karibu na bega lake, akisema angekuwa radhi kuwapunguzia chakula watoto wake mezani, kusudi wajenge mahali ambapo wangeweza kukaa na kuabudia, kidogo ilikuwa ni vigumu kwangu kustahimili. Kwa hiyo mimi na Ndugu George tukaungana na kuamua tungekaa na kuijenga maskani.

Ndipo wakati maskani ilipojengwa, daima ilionekana ... Ile asubuhi niliyoiweka wakfu maskani, ono lilitokea, ambalo limeandikwa na limo mle kwenye jiwe la pembeni, wakati Roho Mtakatifu aliponiambia, “Hii siyo maskani yako.” Mnaona? Basi nikauliza mahali maskani yangu ilipokuwa, ndipo Yeye akaniketisha

chini ya mbingu angavu za bluu. Na ndipo Yeye akasema, "Fanya kazi ya mwinjilisti," na kadhalika, kama mjuavyo. Imeandikwa hata kwenye vitabu.

7 Mambo hayo yote yakiwekwa pamoja. Ndipo siku moja wakati nilipokuwa nikikata nyasi uani kule juu ambako Ndugu Wood anaishi sasa, naye mama mkwe wangu aliishi kule wakati huo; niliketi kwenye kipandio cha nyuma, kipandio kidogo cha kale cha saruji, ambapo nilikuwa nimepajenga mahali hapa padogo kwa ajili ya mama mkwe wangu. Naye kwa namna fulani alikuwa ni bawabu wa kanisa wakati huo, akilishughulikia. Na kwa udhahiri tu kama mtu yeyote angaliweza kunena, Sauti ilinena nami, ikasema, "Kamwe siwezi kukubariki mradi tu unakaa hapa. Huna budi kujitenga na watu wako na mahali hapa. Vema, mimi ... hilo lilinirarua vipande -vipande kwa karibu juma moja au zaidi.

8 Daima, wakati wote, kitu Fulani kimenionya, "Ondoka, ondoka. Elekea upande wa magharibi. Endelea kwenda magharibi." Vema, mimi ... Daima limenisumbua. Na inaonekana kama kila wakati ...

Sasa, nilikuwa nimeamua wazi niani mwangu ya kwamba juma hili niruke kwa ndege hadi Tucson, ambako nilikuwa nikodi mahali, niwe huko kwenye msimu huu wa baridi kali; kuwapeleka watoto shuleni, kuanzia Septemba. Nilipapata mahali hapo. Hata kulikuwako na mahali nilipopewa kule. Lakini kuna kitu ambacho ... Na—na kama nimeondoka ...

9 Jambo lingine ningetaka kusema. Kabla tu hatujajenga nyumba hii hapa juu, ya mchungaji, mahali ilipo sasa, sikutaka kujenga pale. Mama yake mke wangu alikuwa amezeeka. Na hata alilia kuhusu jambo hilo, akasema, "Kamwe siwezi kumwacha mama hapa, huku nikijua yeye ni mzee, na huenda asihudumiwe." Vema, nilielewa hilo. Ninaelewa. Huyu ni mama yake, na ndiye mama pekee aliyepata kuwa naye, ama atakayepata kuwa naye. Kwa hiyo, nilielewa hilo. Kwa hiyo ni—nikamwomba Bwana; Nikasema, "Bwana, kwa kuwa sipendi mahali hapa," nikasema, "nifanye niridhike." Nitaenda popote utakapotaka niende, kutoka mahali popote. Bali sitaki kumhuzunisha mke wangu, kumwondoa hapa, nimpelike nchi ya kigeni ambako hamjui mtu yeyote. Halafu mimi huwa safarini wakati wote, hata hivyo. Nifanye tu nimeridhika kuwa hapa pamoja naye.

Na sasa, wakati mama yake amechukuliwa, naye ameenda Utukufuni, basi hii hapa hiyo shauku inakuja tena, mnaona, sasa ya kuhama. Sijui la kufanya.

10 Na basi hivi majuzi wakati fundisho hili ambalo ndugu walikuwa wamelianzisha huku, nilisimama kutoka mimbarani mara ya mwisho nilipokuwa hapa na kuwaambia ya kwamba nisingekuwa hudumani mradi tu hilo lilikuwa linaendelea. Kwa hiyo, hao ndugu kwa rehema walilinyosha hilo lote. Lote limekwisha. Katika muda wa saa ishirini na nne, lilikuwa limekwisha.

Sasa hilo linanifungulia uwanja tena. Sijui la kufanya. Sijui nigeukie upande gani. Nimemwomba Bwana anipe ono. Nimemwomba aniambie la kufanya. Bali ananiacha tu niketi.

11 Sasa, jana usiku wakati nilipowaondoa watoto wote, mke wangu na wote hao, kutoka nyumbani, nilimtolea Bwana Mungu ahadi. Ndipo nikamwambia Bwana Mungu, "Kama utanibariki katika njia niendayo, nitakutumikia. Lakini itakubidi kunionesha mahali pa kwenda, na jinsi ya kwenda, na jambo la kufanya." Kwa hiyo nilijikabidhi kwa Bwana. Pamoja na—pamoja na huduma na yote, niliikabidhi kwa Bwana. Nami nikasema, "Popote utakapofungua Wewe, chochote ufanyacho, nitatembea katika njia hiyo. Mpaka utakapofanya njia, nitaendelea tu jinsi nilivyo mpaka utakapofanya njia." Nami nikamwomba aifanye dhahiri sana hata sitadanganyika basi, kwa kuwa kweli ninaamini tuko kwenye njia panda za jambo fulani kutukia.

Nilisikia likitabiriwa asubuhi ya leo hapa na Ndugu Neville, ama alilitoa ambapo nilijua lilikuwa—lilikuwa ni unabii aliokuwa akiurejea. Sasa, kwa hiyo, nimewaombea ninyi nyote, nami nawatakeni nyote mniombe, ili kwamba Roho Mtakatifu ataniongoza mahali hasa ninapopaswa kwenda, yale ninayopaswa kufanya, kusudi nisifanye kosa lolote.

12 Mnaona, mara nyingi, watu wanafikiri ya kwamba karama ya unabii, kwamba Mungu husema tu "Nitakuchukua papa *hapa*, na kukuweka *hapa* chini. Sasa, nenda moja kwa moja *hapa*." Wala Yeye huwaambii mambo hayo yote. Kama angekwambia, basi wewe ulikuwa na imani gani ya ushindi? Mnaona? Mnaona, wewe, Yeye hukuacha usimame peke yako kuliko mtu mwingine yeyote. Mnaona? Ninyi nyote mnaweza kunijia na kuniomba mambo fulani, na Yeye kamwe hajashindwa bado ila amewapa jibu. Hiyo ni kweli. Naam. Lakini mimi ninaweza kumwomba mambo yangu ya binafsi, na mara nyingi Yeye huniacha tu peke yangu, mnaona, ananiacha tu niendelee na kuingia humo.

Nina mambo sasa ambayo inanibidi kuyatatua mwenyewe, na maamuzi yanayonibidi kufanya. Na hili ni muhimu sana, mpaka siwezi kulifanya mpaka niwe na hakika ya kwamba ni Yeye anayesema na mimi. Nami ni—ni ... Yeye hatanipa ono. Yeye ananiacha tu peke yangu. Kwa hiyo nimekaa tu kama yatima, kitu kama hicho, asubuhi ya leo, si—sijui nielekee wapi. Kwa hiyo nimelikabidhi kwa Bwana.

13 Ni—nilijisikia kwamba basi, katika kuota hivyo, inanibidi kurudi hapa maskanini na kumsaidia Ndugu Neville mpaka jambo lingine litakapotukia safarini. Kwa hiyo, nitakuwepo.

Nilimwuliza Ndugu Neville dakika chache zilizopita, “Kanisa lilikuwa likiendeleaje?” Naye akasema, “Vema.”

Na kwa hiyo ninasikia ya kwamba mngali mna karama za kiroho na kadhalika miongoni mwenu, ambazo zinafanya kazi, karama za unabii, na—na kunena kwa lugha, na kufasiriwa kwa lugha, ambako ndio kwanza tusikie muda mfupi uliopita. Na mambo hayo yanaliyenga kanisa na sana ...

14 Lakini nilifikiri, labda usiku wa leo huenda, kama Ndugu Neville ... Kama Roho Mtakatifu hatatuongoza kwenye kitu kingine, usiku wa leo ningetaka kuwa na ... Ninyi nyote, kabla hamjaondoka asubuhi hii, mjiandikie swali na kuliacha hapa, swali fulani moyoni mwenu, kusudi tupate kujua kile kanisa linachowazia. Karibu hiyo ndiyo njia waliyo nayo wachungaji ya kutafuta kujua kile kilichoko moyoni mwa watu. Na kila mmoja wenu aliye na swali, liandike na uliweke hapa juu. Kama huna kipande cha karatasi cha—cha kuliandikia asubuhi ya leo, basi liandike usiku wa leo, mapema. Kwa hiyo, ningetaka kuwa na wakati mwingi niwezao, juu ya hayo, kuyachunguza na kuwajibu Kimaandiko.

15 Halafu Bwana akipenda, kama yakiwa ni mapenzi ya Mungu; nimetoa tamshi hapa si muda mrefu uliopita, kwamba ningetaka kuwazungumzia juu ya ile Mihuri saba ya mwisho ya ninii—ya Ufunuo. Sasa, kama sisi ... Nisingeweza kuipitia hiyo Mihuri yote mwaka huu, kwa kuwa inachukua kutoka mlango wa 6 wa Ufunuo, hadi—hadi mlango wa 19, kuimalizia Mihuri hiyo. Lakini ile mitatu ama minne ya kwanza ingeweza kujibiwa katika usiku mmoja, nafikiri, kila Muhuri ukichukua usiku mmoja.

16 Sasa, kama tunaelewa, tazama mahali tunapokomea kwenye Kitabu hicho cha Ufunuo, ambapo Kanisa lilitwaliwa juu Utukufuni. Halafu hayo mengine yanashughulika na Wayahudi, siyo Kanisa hata kidogo. Yanalishughulikia taifa la Kiyahudi. Kwa hiyo hatuna budi kushuka tena chini, kutoka kwenye kule Kunyakuliwa kwa Kanisa, na kuchukua... Tunaona hapa yanayotukia wakati wa Mihuri hiyo, na wakati wa Kanisa la Kimataifa, Kanisa likiisha kuondoka; na pamoja na taifa la Israeli, linashuka na kurejea nyuma na kuwaleta Israeli kutoka wakati lilipowaacha, kufikia wakati wa sasa; na Masihi ajaye, wakati watakapompokea Masihi.

Sasa, mnalipata? Kanisa linanyakuliwa. Mungu alishughulikia kwanza kanisa, nyakati za kanisa. Tulizichukua hizo. Ndipo kanisa linachukuliwa juu katika utukufu. Ndipo Roho Mtakatifu anarudi nyuma na kuwachukua Israeli, kama taifa. Na kuwaleta umbali huu, wakati ile Karamu ya Arusi ikiendelea, kisha anawarudisha tena mwishoni mwa wakati huo. Nitaweka ubao wangu juu, na niweze kuchora na kufundisha, wakati ukifika. Ndipo Bwana anarudi pamoja na Bibi -arusi, na Israeli wanamwona. Na, loo, huo utakuwa ni wakati ulioje.

17 Sasa, kabla hatujalifunga hili kwa usahihi, kuna somo kubwa ambalo ni kikwazo kwa wanatheolojia na waalimu wengi kote katika wakati, na watu wa Church of Christ na wale wanaokuja kulisikia hili, hilo ni, yale Majuma Sabini ya Danieli. Tuna ... Hatuwezi kuendelea mbele katika Ufunuo mpaka tutakapomfunganisha Bibi-arusi na Israeli pamoja na yale Majuma Sabini ya Danieli. Na labda, Mungu akipenda, ili kwamba kama akizungumza nami katika siku za usoni, kuzungumza juu ya baadhi ya haya Majuma Sabini...ama, sio Majuma Sabini, bali Mihuri saba ya mwisho. Halafu Jumapili ijayo, nitajaribu kuchukua Majuma Sabini ya Danieli, Jumapili ijayo, Bwana akipenda. Na kisha hayo yatafungua milango basi, kama Yeye akituongoza, kuanza na hayo mengine. Vema, tutaona kutoka hapo na kuendelea.

18 Mimi pamoja na Ndugu Neville tutafanya kazi pamoja juu ya jambo hili, na kufanya kila kitu tuwezacho kwa manufaa ya watu.

Sasa, tukirudi nyuma kila wakati, tunawaombea wagonjwa, daima tuna furaha kufanya hivyo. Na labda nitafanya hivyo kila mkutano, kama watu ni wagonjwa, kuwaombea.

Sina hamu ya kufanya upambanuzi wowote zaidi. Mnaona? Sasa, hili ndilo lililotukia. Nimejaribu. Nami ninajua nimefanya mambo ambayo ni makosa; bali nimejaribu kuishi karibu na Mungu vya kutosha, wakati wote, kwa Mungu, hivyo ndivyo maono haya yangetukia, jinsi ambavyo yangetukia. Hata watu wangepoteza vitu, nao wananiita, wananisihini niwaombea kwa Bwana, kuulizia mahali kilipokuwa. Kama vile Yese alivyowapoteza wale nyumbu, nao wale vijana wakashuka wakaenda kumtafuta nabii, naye akawaambia ambapo hao nyumbu walikuwa tayari wamerudi nyumbani. Hilo ni sawa kabisa. Lakini linazidi sana, watu wengi sana... Siyo tu katika eneo kama hili; ni kote ulimwenguni, mnaona. Mnaona? Kwa hiyo inakuwa tu, linanitazita sana, halafu linakutia wasiwasi wakati wote, mpaka inafikia mahali...

19 Na hiyo ndiyo iliyowafanya hao ndugu kuanzisha hilo fundisho, ya kwamba nilikuwa Bwana Yesu Kristo aliyefanyika mwili. Nasi tunajua ya kwamba hilo lingearua Huduma hii yote vipande-vipande, na kuleta dhihaka juu ya Kristo na kila kitu. Mnaona? Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu ilinibidi kuwatikisa vikali, waliache mara moja, kuwafanya wajue ya kwamba hilo halikuwa ni la Mungu, hilo lilikuwa ni la ibilisi. Mnaona? Nao ni watu wazuri. Na ilionyesha watu hao wamezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, kwa sababu, walipoiona Kweli kwa Maandiko, walimrudia Mungu, hakika, mnaona, mara moja. Kwa hiyo hiyo ilionesha ilikuwa ni Shetani akijaribu kufanya jambo fulani na watu; wote walikuwa Wakristo wacha Mungu.

20 Na iliwafanya wengi wao kuniambia, "Ndugu Branham, tuna imani zaidi na wewe sasa kuliko tulivyopata kuwa nayo."

Maana, mnaona ni nini, kwa karama ambayo Mungu amenipa, ningaliweza kufanya nini na hiyo? Nililitupa taifa miguuni pangu, ama, watu. Kile tunachoita taifa, siyo "ulimwengu" hapa nje, kile—kile chakula cha mizinga na kadhalika, ninamaanisha Wakristo, mwaminio halisi, hao ndio walio bora kuliko wote wa ninii... Tunazungumza juu ya *taifa*, tunahubiri juu ya watu waliozaliwa mara ya pili; hilo ndilo tunalolizungumzia taifa. Si kila mtu tu hapa nje, ambao ni wachafu sana na vinyaa ambao tunaishi ulimwenguni, hao ni—hao ni mavumbi tu ya duniani yanayorudi. Ninazungumza juu ya Wakristo waliozaliwa mara ya pili, watu ambao ni Wakristo halisi.

21 Ninamngojea mtu anirukie tena juu ya jambo fulani. Mtu mmoja alinjia sio muda mrefu uliopita, na kusema, "Wazo lenyewe, la Kristo akitema mate ardhini, kwa mate Yake, na kufanya tope na kulipaka machoni mwa mtu fulani." Kasema, "Huo ulikuwa ni uchafu, kinyaa jinsi gani, Kwake kutema mate, kwa mate yake kutoka kinywani Mwake! Ilikuwa ni kukosa usafi jinsi gani, kutema mate ardhini, na kufanya malundo ya matope na kuyapaka machoni mwa mtu." Nikasema, "Lakini alirudi akiona." Mnaona, jambo ndilo hilo.

Na mtu yule yule ... Walifungua kambi ya wenda uchi huko juu karibu na kwangu, mwajua, kidimbwi cha kuogelea. Na—na mtu huyo anayo tiketi kwa ajili ya kila mmoja wa watoto wake waende kule na kuogelea kwenye kidimbwi kile. Naye na mke wake huenda, pia. Katika kidimbwi hicho ... Samahani, dada zangu. Lakini ambapo hao wanawake mle ndani wakiogelea, karibu mia moja, ama mia mbili, kila siku; wanawake, uchafu huo wote na kadhalika, na wanawake siku hizi, na wakiogea mle katika hayo maji, uchafu huo na kinyaa vinywani mwao, na kuyameza na kuyatema. Ninamtaka tu anirukie, mnaona.

Wao walisema, "Kama—kama Kristo alikuwa akiishi leo hii, wangemtia mbaroni kwa sababu ya jambo hilo la kukiuka kanuni za afya."

Vipi kuhusu *hilo*? Nina hakika mnafahamu ninalomaanisha. Wanaingia moja kwa moja kwenye kidimbwi hicho, na wengi wao wakiwa na magonjwa, kaswende, kisonono, na cho chote kile, papo hapo. Nawe unayatema tu kwa kinywa chako, na kila kitu namna hiyo, na kuoga mle ndani namna hiyo ... Na huo ni usafi, bila shaka?

22 Kwa hiyo, loo, jamani, siku hii tunayoishi, ndugu, dada, ni wakati wa kuja kwa Bwana. Ni—ni ... Kanisa lina tumaini moja: huko ni kuja kwa Bwana.

Vema, siwezi kukomesha mambo hayo; hakuna haja. Biblia ilikwishatabiri yangekuwapo hapa. Siwezi kuyakomesha. Bali ninataka sauti yangu iwe kwenye kumbukumbu Mbinguni, ya kwamba niliyapinga. Wakati wa ile Hukumu utakapofika, nilikuwa nikipinga jambo hilo.

Bado ninaamini ya kwamba Biblia hii ni Neno la Mungu. Na hakuna kitu kingine ulimwenguni, kinyume Chake, kinachoweza kukomesha jambo Hilo. Lakini Biblia hii hapa, hii ni Kweli; hili ni Neno la Mungu. Kwa hiyo sasa na tutweke matanga ye—ye—yetu, na tutie nanga kidogo kwenye pwani iliyotulia ya Mahali pa Raha. Na—nasi tunaweza kusafiri kesho mahali fulani, lakini hebu na tutie nanga sasa na kuisikiliza Sauti ya Baba yetu wa Mbinguni wakati akinena na sisi kupitia kwenye Neno Lake, tunatumaini, leo.

23 Na usiku wa leo, sasa, tengenezeni swali lolote dogo mlilo nalo kuhusu ... Sasa, si kitu kitakachomdhuru mtu fulani. Kama ukifanya hivyo, basi hiyo ni ... Nisingejibu hilo kwanza. Mnaona? Lakini wewe, kitu fulani, tuseme, "Vema, sasa, kama nikifanya jambo fulani, je! Mungu anasema tunapaswa kufanya jambo hili?" Ama, unajua, maswali madogo moyoni mwako. Ama, "Tuna karama zinazofanya kazi kwetu, Ndugu Branham, na je! tuzifanyie kazi *hivi* ama *vile*? Ama, tufanye nini?" Jambo fulani ambalo ningeweza kukujibu katika Maandiko. Mnaona? Andika kitu kidogo, ningefurahi. Na kama hakuna, basi nitachukua tu somo la namna fulani, na kuwahubiria usiku wa leo, Bwana akipenda. Hii ni Jumapili, nami nimekuwa ...

24 Jumapili iliyopita nilianza kwenda kwa Ndugu Cauble. Nami nikasikia kengele hii ya kanisa ikilia, nami nikatembea tu huku na huku uani. Nisingeweza kuvumilia jambo hilo. Hivyo tu. Niliwasikia, kwa hiyo i—i—ilinibidi tu kushuka kuja hapa.

Kwa hiyo sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa na kunena na Muumba wetu, na halafu katika maombi madogo. Kuna mtu aliye na haja maalum? Inueni tu mikono yenu, semeni tu, "Mimi ..." Fanyeni tu ijulikane. Mungu anajua yaliyo moyoni mwako. Sasa, weka tu ombi lako moyoni mwako.

25 Mungu Mtakatifu sana, Ambaye ameumba mbingu na nchi kwa Neno la kinywa Chako, kwa mawazo ya nia Yako. Tunakuja katika Uwepo Wako, kupitia Yesu Kristo Bwana wetu, kukushukuru kwa ajili ya yote ambayo umetufanyia. Nasi tunakushukuru sana, Bwana, asubuhi ya leo kujua mahali tunaposimama, kujua mahali tulipo asubuhi ya leo, na historia ya wakati, na wakati ujao unaokuja. Tukijua leo hii, ya kwamba kwa neema ya Mungu, ya kwamba tumeoshwa katika Damu ya Kalvari, ya kwamba tumejiandaa, tukiwa na imani mioyoni mwetu, kumlaki Yeye ikiwa angekuja leo hii. Tunapaswa kusema, "Hata hivyo,

njoo, Bwana Yesu.”

Nasi tunaona dhambi ikilundikana, mpaka inaonekana kana kwamba ulimwengu unayumbayumba chini ya matokeo ya dhambi. Jinsi ambavyo kunywa pombe na kucheza kamari, na karamu za ulevi, na uchi, na, Ee Mungu, uchafu, na taka na kinyaa cha watu, na jinsi ambavyo wao, laiti wangalitambua ... Bwana, Je! watu hao, wanaovalia jinsi hiyo katika maskini nguo hizo chafu zisizo za kitauwa, na wanaenda huko nje mtaani, hivi wanatambua ya kwamba wao si kitu ila wadudu na mavumbi, ambao labda katika juma lingine wadudu watakuwa wakiula huo mwili ambao wanautukuza jinsi hiyo? Hivi wanatambua ya kwamba parare wataula? Nayo nafsi yao itakuwa huko ng'ambo katika Umilele bila ya Mungu, bila ya Kristo, bila ya tumaini, ikitumbukia ndani kabisa katika kufa moyo, wapate kuangamizwa kabisa katika Kuja Kwake? Ee Mungu, tupe sauti za—za maonyo, tupate kumwonya kila mtu juu ya hatari hii wanayoikaribia.

26 Uwe pamoja nasi leo hii na utupe “maneno ya hekima,” kama vile Sulemani alivyosema wakati mmoja katika Mhubiri, tuweze kuwa wajenzi wenye hekima, tupate kuwa wachungaji wa kusanyiko hili. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba tunapoyatafuta maneno ya kusema, ya kwamba yapate kuwa—yapate kuwa ni vipeo ambavyo vingeeunasa moyo ulio na haja sana hapa asubuhi ya leo.

Hatujaja na kukusanyika chini ya paa hili lenye joto leo hii, tupate tu kuonekana, bali tumekuwa hapa kwa sababu tunakupenda, na kwa sababu tunatamani kusikia kutoka Kwako. Wewe ni Mpenzi wetu tunayempenda, nasi tunatamani kusikia Maneno kutoka Kwako. Tunashukuru kwa yale tumekwisha kusikia. Yatadumu pamoja nasi kwa muda mrefu. Sasa tupe sehemu uliyo nayo kwa ajili yetu leo, tunapoendelea kukungojea Wewe. Tunaomba katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

27 Sasa, ni ... [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine. Ndugu fulani anafasiri — Mh.]

Tunashukuru kwa ajili ya huku kutukuzwa kutoka kwa Roho, kunatwambia na kutuonya tuyaangalie Maneno ambayo labda Roho Mtakatifu atatumungumzia leo. Nasi hatujui ni kitu gani alichotuwekea akiba, bali tunajua ya kwamba hapana budi kuna kitu fulani atakachotoa. Labda swali limo moyoni mwako, kwamba atalinena kupitia hapo. Huenda akalinena kupitia kwenye Ujumbe asubuhi ya leo. Huenda akalinena usiku wa leo ibadani. Yeye, wakati fulani leo hii, Yeye anajaribu, inaonekana kama, kumwonya mtu fulani ayashike Maneno hayo.

28 Sasa kuligeukia Neno lililoandikwa, hebu twende kwenye Kitabu cha Kutoka, kwa ajili ya somo la Shule ya Jumapili.

Je! Mna ibada ya ubatizo? [Ndugu Neville anasema, “La, hatuna mpaka saa kumi na mbili jioni ya leo.”—Mh.] La. Ibadu ya ubatizo saa kumi na mbili alasiri ya leo.

29 Hebu twende kwenye mlango wa 17 wa Kutoka, na tuanzia kwenye—kwenye kifungu cha 5, ninaamini, kifungu cha 5 na cha 6 cha mlango wa 17 wa Kutoka.

BWANA akamwambia Musa, Pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende.

Tazama, nitasimama mbele yako...juu ya ule mwamba huko Horebu; na...utaupiga mwamba, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli.

Sasa kama ningeliita hili somo dogo la Shule ya Jumapili, ningetaka kuchukua hili kama somo la asubuhi ya leo, *Maji Yaliyopo Daima Yatokayo Mwambani*.

30 Tunajua ya kwamba Israeli daima imekuwa mfano wa kihistoria wa kanisa. Kwa sababu Israeli walikuwa watu wa Mungu mpaka walipotoka Misri, na ndipo walikuwa kanisa la Mungu kwa sababu walikuwa wametengwa na ulimwengu mwingine.

Na wakati tunapotenganishwa na ulimwengu mwingine, ndipo tunakuwa kanisa. Lakini mradi tu tumeshikwa na ulimwengu mwingine, basi hatuko kanisani. Sasa, natumaini ya kwamba hilo linaingia ndani kabisa, linashika mahali pake. Mnaona, sisi si kanisa mpaka tumejitenga na ulimwengu. Kujitenga wenyewe, kutoka miongoni mwa watu wachafu, tusiwe na uhusiano nao, wala tusizishiriki dhambi zao. Usifungwe nira pamoja na wasioamini, bali jitenge na mambo ya ulimwengu.

Na wakati Israeli walipokuwa Misri, walikuwa watu wa Mungu. Ndipo wakati walipoitwa watoke, ama walipokuwa na kule kutoka, wakitoka nje, basi waliitwa kanisa, kwa sababu hapo ndipo walipojitenga wenyewe na walimwengu wengine.

31 Nalo neno lenyewe “kanisa” linamaanisha “walioitwa watoke.” *Kutoka*, “kutoka nje.” Kila mmoja wetu, kama Wakristo, tumekuwa na kutoka maishani mwetu. Tulikuwa na wakati ambapo tuliitwa kutoka miongoni mwa wenzetu, tukaitwa kutoka miongoni mwa watu ambao wakati mmoja tulishirikiana nao, na

kuwa watu tofauti, kutembea na watu mbalimbali ambao walitenda kwa njia tofauti na kuzungumza kwa njia nyingine. Ilikuwa ni kutoka katika maisha yetu.

Mfano mzuri sana ambao Israeli ilitupa wakati Mungu alipowaita watoke. Walikuwa na kutoka, nao wakatoka miongoni mwa wa—watu wa ulimwengu, wakawa taifa lililotengwa, kwa Mungu, watu wa kipekee. Walitembea chini ya vivuli vya kiti cha rehema. Waliishi na kutembea karibu na ile Nguzo kuu ya Moto. Na Mungu akawatoa Misri akawaleta kwenye nchi ambayo alikuwa ameahidi.

32 Na katika kutoka huku, walipewa kiongozi wa kiroho, kiongozi, ambaye alikuwa ni Musa, nabii mkuu aliyetiwa mafuta ambaye alikuwa m—mtu mashuhuri. Yeye alikuwa mtu mcha Mungu; alizaliwa mtu mcha Mungu. Mungu alimwita kutoka kwa mama yake, hata kabla ya wakati huo; Mungu alimchagua kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, apate kuwa kiongozi wa kizazi hicho, kuleta huku kutoka kwa watu.

33 Hapa wakati fulani uliopita, nilizungumza na watoto wadogo hapa maskanini, nami nilikuwa na mahubiri madogo kwa ajili yao; na kuwaambia, ama kutoa mfano mdogo wa jinsi ambavyo Yokebedi, jinsi alivyoomba, yeye na Amramu, baba yake Musa, kuhusu kufanya jambo fulani kuhusu kuwakomboa watu hao. Ndipo Amramu akaona ono la Mungu amesimama, ama Malaika, akielekeza kaskazini, na akamwambia kile ambacho kingetukia. Ndipo mtoto Musa akazaliwa. Wala hawakuogopa amri za mfalme, wala vitisho vyake. Walijua ya kwamba Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya Musa, na hilo lilitosha. Hiyo ni kweli. Haijalishi mfalme alisema nini, kile ulimwengu wa kisiasa ulichosema, kile kitu kingine chochote kilichosema, wao walijua Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya Musa. Kwa hiyo hawakuogopa kumwachilia, moja kwa moja katikati ya mamba; wakati wote walipokuwa wamenona kwa watoto wa Kiebrania, ambapo walikuwa wamewatoa kule wakaliwa na mamba. Na hata hivyo Musa aliwekwa moja kwa moja ndani ya kijisafina kidogo na kupelekwa huko nje moja kwa moja miongoni mwa hao mamba, moja kwa moja kati yao. Kwa sababu hawakuogopa kitu; walijua ya kwamba Mungu alikuwa ameweka mkono Wake juu ya Musa.

34 Vema sasa, kama tungejua tu jambo lile lile, ya kwamba Kiongozi wetu mkuu, Roho Mtakatifu, Mungu amemtuma, Naye ni Kiongozi wetu. Na haidhuru ulimwengu unasema nini, na jinsi wanavyokucheka na kukudhihaki, sisi tunamfuata Kiongozi wetu. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kuwa Kiongozi wetu. Mnaona? "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena. Hata hivyo mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Kwa hiyo Kiongozi wetu mkuu yuko pamoja nasi, Roho Mtakatifu. Sasa, hatuna budi kumfuata Kiongozi huyu na kutenda kama Yeye anavyosema tufanye. Na Kiongozi huyu kamwe hatatuondoa njiani, Yeye atatuweka moja kwa moja kwenye njia ya Maandiko wakati wote. Lakini kamwe hataenda upande mmoja kwa ajili ya jambo fulani, na upande huu kwa jambo fulani. Yeye atakaa moja kwa moja katika njia ya Maandiko.

35 Naye Musa alikuwa na njia aliyokuwa awapitisha Israeli, na waifuate moja kwa moja waivuke Bahari ya Shamu, moja kwa moja wauvuke Yordani, waingie moja kwa moja katika nchi ya ahadi, moja kwa moja kupitia jangwani. Haikuwa ni Musa aliyeeondoka kwenye mstari. Haikuwa Mungu nje ya mstari. Ni watu walio nje ya mstari ndio waliosababisha shida. Kwa hiyo hebu na tufikirie mambo haya sasa. (Samahani.)

Musa, kiongozi huyu aliyetiwa mafuta ... Hatimaye, alipokwisha kuwaonesha hao watu kwa ishara na maajabu, ambayo Mungu peke yake Ndiye angaliweza kuyafanya ... Alifanya ishara hizi na maajabu mbele ya wazee wa Israeli, na mbele ya Israeli, mpaka wakaridhika ya kwamba huyu Musa alikuwa ndiye mtiwa mafuta ambaye alikuwa awatoe kwenye nchi hii, awapeleke kwenye ile nchi nzuri ambayo walikuwa wameahidiwa. Ndipo walipoona mambo haya makuu ambayo Musa aliyafanya katika jina la Mungu, walikuwa radhi kumfuata. Ndipo akawatoa, na kuwaongoza kupitia kwenye Bahari ya Shamu, wakaivuka, walikuwa kwenye nchi kavu, na safari ya kuingia jangwani, ambayo inamaanisha wakati wa majaribu.

36 Wakati mtu anapompokea Kristo kama Mwokozi wake, kila kitu kiko juu ya nyumba. Lakini, kabla mtu huyu hajaingia kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu; mtu huyu, hana budi kwanza kuwa na mchakato wa utakaso. Hana budi kuwa na wakati wa kujaribiwa maishani mwake. Nyote mlikuwa nao. Alikuwa na wakati huu wa kujaribiwa. "Kila mwana amjiaye Mungu, kwanza anateswa, anarudiwa, anaadhibiwa. Na endapo hatuwezi kuyastahimili marudio, basi inaonesha sisi si wana wa Mungu; tu wanaharamu, wala si wana wa Mungu," Biblia ilisema. Lakini kama tunaweza kustahimili kurudiwa, tukijua ya kwamba "mambo yote hutenda kazi pamoja kwa manufaa ya wale wampendao Mungu," ndipo sisi ni wana na binti za Mungu, ndipo Yeye anatutia muhuri kwa Roho Mtakatifu hata siku ya ukombozi wetu. Mnaona, huko ni kurudiwa, majaribu, jambo tunalopitia.

Nao Israeli, kama mfano wa kihistoria, iliwabidi kuyastahimili marudio haya.

37 Sasa, wakati walipokuwa huko chini Misri, ndipo Mungu akamtuma Musa basi aliinyosha fimbo, na viroboto na chawa wakaja ardhini. Akanyosha kuelekea jua, nalo likatua. Yeye aliunyosha juu ya maji, nayo yakageuka yakawa damu. Mbona, Waisraeli walikuwa huko Kanaani...huko katika—katika Gosheni, wakiwa tu na wakati mzuri; jua kamwe halikutua, mapigo kamwe hayakuwapiga; mbona, walikuwa tu na wakati mzuri, ni kama tu ulivyofanya wewe wakati ulipookolewa kwa mara ya kwanza.

Kila kitu, ndege waliimba tofauti, na kila mtu alikuwa mtamu. Na, loo, jamani, jinsi kila kitu kilivyokuwa vizuri sana wakati ulipookoka kwa mara ya kwanza. Ndipo ukaja wakati wa majaribu, kurudiwa, wakati wa kutakaswa, kujitakasa na mambo ya ulimwengu, “ukiweka kando mizigo ikuzingayo kwa upesi.” Wewe, mwanamume, ilikubidi kuacha uvutaji wako wa sigara, kuacha unywaji wako wa pombe, kuacha kwenda kwako kwenye chumba cha kucheza kamari, karamu zako za usiku kucha za kadi. Mambo hayo yote, ilikubidi kujitakasa kutokana nayo, kwa imani katika Damu ya Yesu Kristo, kujitakasa. Ninyi wanawake iliwabidi kuacha nywele zenu zikue, kuzirefusha nguo zenu, na kutenda tofauti na jinsi mlivyokuwa, wakati wa kutakaswa! Mara nyingi wangeasi na kurudi nyuma; vema, huyo si mwana wa Mungu. Mnaona? Mtoto wa Mungu anaangalia moja kwa moja Kalvari na anajua ya kwamba ni kwa manufaa yake.

38 Kwa hiyo basi kipindi hicho cha wakati, hapo ndipo kule kuanguka kuuu kulipokuja katika Israeli. Wakati huu msongamano mkubwa, basi watu walianza kuanguka kutoka upande mmoja hadi mwingine. Ndipo katika mazungumzo yao, “Vema, laiti tungalikuwa tumerudi huko Misri. Nafsi zetu zinauchukia mkate huu mwepesi. Kwa maneno mengine, kama ningalichukua kihistoria sasa, hivyo ndivyo walivyosema.

Sasa, katika siku za kisasa, ingekuwa, “Loo, kila Jumatano usiku, mkutano wa maombi. Kila Jumapili asubuhi, tunarudi kanisani. Tunasikia nini? Kitu kile kile; mhubiri anasimama na kuhubiri; nyimbo; endelea kurudi.” Mnaona, basi unaenda tu kama wajibu. Wewe si mwabudu. Mwabuduo huenda kule kuabudu, kujieleza mbele za Mungu wake, kumsifu Mungu kwa ajili ya wema Wake; kwa kila Neno, yeye anajishikilia Kwalo.

39 Ni kama tu mapenzi. Kama ulikuwa ukiandamana na msichana kwa sababu ulijua ilikuwa ni wajibu, ama unaambatana na mvulana, wakati ulipokuwa kijana ... “Mama ananitaka niambatane na jamaa huyu, bali hata kamwe siwezi kumvumilia.” Hupati chochote kwake yeye kuja kukuona. Ama, kama ni vile vile kuhusu msichana kwa mvulana, ama mvulana kwa msichana. Unaambatana naye, anakuchosha; mama anakutaka uambatane naye kwa sababu yeye ni aina ya msichana ambaye mama anampenda. Mnaona, anakuchosha; hakuna mapenzi. Lakini wewe hujali, hutaki kuoga, hutaki kwenda kumwona. Nayo ni ninii ... Mbona, ni jambo la kuchukiza sana. Na wakati anapokuja kukuona, jamani, unatamani tu angaliondoka upesi, aende zake nyumbani.

Hivyo ndivyo ilivyo wakati wewe, “Ni kwa nini yeye anahubiri kwa muda mrefu hivi? Na vipi kuhusu mambo *haya* yote, na kila kitu?” Mnaona, wewe huna mapenzi.

Lakini wakati kweli unapolishikilia kila Neno, kama Roho alivyowapa onyo asubuhi ya leo, (Mnaona), “Kushikilia kila Neno ...” Huenda hilo likawa ndilo ambalo amekuwa akiwazungumzia juu yake, kushikilia. Ni Uzima wa Milele, kila Neno la Mungu. Ni furaha kwenda kanisani, chini ya hali yoyote. Kama kuna joto, baridi, vuguvugu, kama watu wanazozana, wananung'unika, chochote wanachofanya, ingali ni furaha kulisikia Neno la Bwana. Ndipo unampenda Kristo basi, (mnaona?); unampenda kwenda kanisani.

40 “Vema, mpenzi, hii hapa Jumapili asubuhi tena, ninadhani hatuna budi kuwaogesa watoto na kwenda kule chini. Jamani, inachosha.” Mnaona, wewe humpendi.

Lakini kama kweli unampenda, huwezi tu kungojea hata Jumapili asubuhi ifike; inakubidi tu kushuka kule chini pamoja nao. Nasi tunafika, na kuondoka... Watu wa Mungu, hawakuchoshi. Mbona, wao ni—ni ndugu na dada. Kama nilivyokuwa nikisema, “Unakuwa mnene kama molasi ya Mtama kwenye asubuhi yenye baridi.” Hai—haitiririki, inakaa tu pamoja, mwajua, inashikana kabisa. Sasa, huo ni msemo jeuri, lakini ni—ni—ni kujaribu kuwajulisha kile ninachomaanisha, mnaona. Mnaona? Mnashikamana. Na kadiri inavyozidi kuwa baridi, ndivyo wanavyoshikana kwa nguvu zaidi. Na hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa kwetu sisi. Kadiri inavyokuwa baridi...

Marafiki wa duniani wanapokuacha,
Bado endelea kumshikilia Yeye zaidi.

41 Na kile tunachopendana, mmoja kwa mwingine, si kwa sababu sisi ni mtu fulani; bali ni Kristo ndani ya kila mmoja wetu, ndiye tunayempenda. Mnaona? Ni yule Mungu aliye ndani ya utu wetu, Ndiye tunayempenda. Sasa tunapenda kukusanyika pamoja tulizoea kuuimba ule wimbo wa kale:

Kibarikiwe kifungo kinachofunga
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ili nia ya ushirika wa kindugu
Ni kama ile ya Juu.

Unaona, ushirika wa watu wenye nia moja ni kama ule wa Juu.
Mbele ya kiti cha enzi cha Baba yetu,
Tunamwaga maombi yetu ya dhati;
Woga wetu, matumaini yetu, malengo yetu ni moja,
Faraja zetu na tegemeo letu.

Mnaona? Naam, bwana. Wakati mtu amekuwa na baraka, sisi sote tuna furaha kuhusu jambo hilo.

Mtu anapohuzunika, tunasikitika pamoja naye. Tu—tunataka sote tuwe pamoja. Sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kuwa.

42 Na hivyo ndivyo Israeli walivyopaswa kuwa. Lakini ukawa ni mzigo, "Loo, maskini mkate huu mwepesi, mkate wa Malaika ... Vema, tunajali nini juu ya mkate huu mwepesi? Nafsi zetu zinakichukia kitu hiki. Na kila kitu ni kosa. Na—na maskini mana hii ya kale inayoshuka kila usiku, mbona, afadhali tule kitunguu saumu na iliki kutoka Misri." Mnaona, mioyo yao haikuwa tayari kwa safari hiyo.

Na wakati mwanamume ama mwanamke anapoanza kulalamika juu ya kwenda kanisani, wanachoshwa sana na kwenda kanisani, hawako tayari kwa ajili ya safari. Hiyo ni kweli. Kuna kasoro mahali fulani.

Loo, mnapompenda Mungu, na mkiwazia mnaenda Mbinguni, nanyi nyote mnaenda pamoja ...
Ni ushirika ulioje, ni furaha ya Kiungu iliyoje,
Egemea kwenye Mkono wa milele;
Loo, ni amani ya heri jinsi gani na Bwana wangu akiwa karibu hivi,
Nikiegemea kwenye Mkono Wake wa milele.

Ni ninii ... Tunaimba nyimbo hizo.
Tunashiriki ole zetu za pamoja,
Tunabeba mizigo yetu pamoja;
Na mara kwa mara mmoja kwa mwingine hudondosheana
Chozi la huruma.
Tunapoachana,
Inatumiza kwa ndani;
Lakini tungali tumeunganishwa moyoni,
Na kutumaini kukutana tena kwenye wakati ujao wa mkutano wa maombi. (Naam, bwana, tungali tumeungana moyoni!)

43 Sasa mnakuwa tayari kwa ajili ya safari hiyo (mnaona?); mko tayari kuingia katika Nchi ya ahadi, nyakati za majaribu. Hilo ndilo eneo la hatari, jangwani, nyakati za majaribu.

Israeli, katika wakati wao wa majaribu, walianza kugombana na kuzozana wao kwa wao, wakiuchukia ule mkate. Nao walitaka kurudi Misri.

Na ndipo wanaanza kulalamika juu ya kiongozi wao. Loo, waliogopa kwamba alikuwa akiwapoteza; baada ya yeye kujionesha kuwa kiongozi, na Mungu alikuwa amethibitisha ya kwamba yeye alikuwa kiongozi. "Vema, labda tumetenda kama washupavu wa dini. Na—na labda tumepotea, sote tukaenda kombo," ama, kitu kama hicho. Mnaona? Walikuwa wakizungumza dhidi ya Mungu na dhidi ya Musa: Mungu na kiongozi Wake.

44 Sasa, tunapofikia mahali, tukisema, "Sijui kama Neno linamaanisha *Hili*, ama la. Nami sijui kuhusu Roho Mtakatifu; Mimi kidogo ninashuku jambo Hilo. Ninajua wengine ambao hawana." Vema, endelea uingie Misri. Mnaona?

Lakini kama kweli umedhamiria kukaa barabarani, kaa moja kwa moja na huyu Kiongozi, Roho Mtakatifu, dumu na Neno. Na kama ukidumu na Roho, Yeye atakuweka katika Neno. Hiyo ni kweli. Yeye atakuchukua moja kwa moja barabarani, njia ya Neno. Tena usimwogope. Hataumiza chochot; atakusaidia tu kama umeumizwa. Atayaponya maumivu yote; Roho Mtakatifu ataponya.

45 Sasa, tunaona ya kwamba, wakiwa njiani, baada ya kuwa hivi, walifika mahali pa Horebu. Na H-o-r-e-b, Horebu, ndipo tunaona ... Hebu na tulichambue jina hilo. Hapo ndipo ji—jina Horebu linamaanisha "mahali pakavu" ama "jangwa."

Na tunapotoka kwenye ushirika mmoja na mwingine kanisani, na kutoka kwenye ushirika na Roho Mtakatifu, inatuleta kwenye mahali pakavu, jangwani, hakuna kilicho hai, kila kitu kina miiba. Mnaona, ja—jangwani, kipande kidogo cha mpungate kikiwa na mwiba. Mlijua hiyo ni nini? Hilo ni jani dogo laini la thamani ambalo halijapata maji, limejisokota tu kabisa hata likawa mwiba. Na unapomwona mtu fulani kama huyo, labda ni nafsi ya thamani ambayo ingelimwagiliwa maji vizuri, ingelikuwa ni jani dogo laini ama chochote kile. Lakini badala yake, limejisokota sana hata likawa ni mwiba, likidunga tu kila kitu, mwajua, likitafuta makosa. Kitu pekee linachohitaji ni maji. Hivyo tu. Linaninii tu linahitaji tu u—uamsho, ama kuvunjika, kuburudishwa kutoka kwa Bwana. Lita—litajifungua lenyewe, kama tu utaliweka kwenye maji.

46 Lakini, hapo ndipo ambapo hao wanaoishi mahali hapo inawabidi kuvumilia hali za mahali hapo. Nao wale wanaotamani kuishi katika mazingira ya aina hiyo, ya mahali ambapo kila kitu ni kugonga tu na kuzozana, na kugombana na kushikwa na kiherehere namna hiyo, vema, utaishi tu chini ya mazingira hayo, hivyo tu. Lakini si lazima tuishi mle, haina haja kwetu kuishi mle.

Sasa, hii Horebu ilikuwa ndipo mahali ambapo Mungu alivunjika moyo kuhusu watu hao, kwa kuwa walikuwa wamezurura mahali hapa nao wakaingia katika hali hii. Naye akawaleta moja kwa moja kwayo,

kwa kuwa wasingetembea kwenye ile njia. Waliondoka kwenye ba—barabara kuu, wakatoka na kuingia kwenye barabara hii ya pembeni. Ndipo ikamfanya Mungu kufanya jambo lililokuwa ni la kuogofya sana. Yeye ... Ikamfanya Mungu kumwamuru Musa aichukue fimbo ile ya hukumu ambayo alikuwa amelihukumu taifa kwayo, na kuupiga Mwamba, utoe maji.

Sasa, pana somo zuri hapa kama tungeweza tu kulipata. Mnaona? Na kwa sababu tumevurugika sana, na kufungwa na ulimwengu, na kadhalika, ilimfanya Mungu kuzichukua hukumu za ulimwengu na kumpiga Mwanawe Mwenyewe kwazo, pale Kalvari, tupate kuwekwa huru. Mnaona ninalomaanisha?

47 Sasa, ili kuwapeleka watu hawa kwenye maji, wakiisha kufika kule, mahali hapa pakavu palifanywa Kalvari. Na hapo Mungu akamwambia Musa, akasema, "Ichukue ile fimbo pamoja na wazee, na mwende mbele, Nami nitasimama juu ya Mwamba mbele zenu." Nao Mwamba huu ulikuwa ni Kristo. Naye Musa, akiwa na ile fimbo aliyoliletea hukumu taifa la Israeli, alichukua fimbo hiyo hiyo na kuzipiga hukumu za Mungu juu ya huo Mwamba. Mnaona? Alichukua dhambi za watu akaiweka kwenye fimbo hii. Ambayo alipaswa kuwapiga watu hao, badala ya kuwapiga watu hao aliupiga Mwamba. Na ule Mwamba, kupitia kazi ya Mungu, ulileta wokovu, ukawaletea watu wanaopotea maji. Ilileta uhai kwa watu wanaokufa. Na hivyo ndivyo Mungu alivyofanya kwa kuichukua fimbo Ya—Yake rasmi ya hukumu, na kuzizungushia dhambi zangu na zako kwenye fimbo hii; wakati ilipaswa kutupiga, bali ilimpiga Kristo; hata kutoka Kwake yakaja maji, ambayo yanamaanisha "Roho." Roho Mtakatifu alikuja toka Kwake, kutupa Uzima. Sasa, tuna Uzima wa Milele. Sasa, Mwamba huu ulikuwa ni Kristo. Sasa, tunataka kuona.

48 Nimeona michoro mingi sana ya kiakili ya Mwamba huu. Niliiona moja ya iliyo makinifu sana, si muda mrefu uliopita, hata palikuwapo na mwa—mwamba mdogo uliwekwa juu ya kilima. Na—na Musa alidhaniwa alikuwa ameupiga mwamba huu, nao Israeli walikuwa kule chini wakiwa na kikombe cha chai, wakijipatia maji kutokana na mnyunyizo mdogo ulioanguka kutoka kwenye mwamba huu. Sasa, hilo ni wazo tu la mtu fulani.

Lakini wakati Mwamba huu ulipotoa maji Yake, kulikuwako na zaidi ya watu milioni mbili, mbali na maksai, ngamia, na kila kitu kinginecho kilichokunywa mapipa ya maji kutoka Kwake. Kilikuwa ni kijito kinachobubujika kilichotoka mle!

49 Hivyo ndivyo wanavyojaribu kumfanya Kristo, Roho Mtakatifu leo. Ni mnyunyizo mdogo tu (Mnaona?), wa kutosha tu kukufanya uamini ya kwamba Mungu yupo. La.

Ni wingi wa Maji. Daudi alisema, "Kikombe changu kinafurika." Ni bubujiko tu la Roho Mtakatifu.

Watu wanaliogopa. Watu wengine husema, "Vema, ninahofu tu kidogo nitafanya *hivi* ama *vile*, ama ikitokea kwamba niingie kwenye kilindi kidogo kupita kiasi. Ninaweza kukuonyesha mtu fulani aliyekwenda umbali mrefu kidogo kupita kiasi." Lakini kamwe huelekezi kwa yule ambaye hakuenda umbali wa kutosha. Mnaona? Naam, vipi kuhusu wale ambao hawakuenda umbali wa kutosha?

50 Sasa, tumekuwa na baadhi ya watu ambao waliingia katika mwili, nao wakaenda kombo. Na—na si Mungu, bali watu wakaninii... Kwa sababu ya ukosefu wa uongozi mwema, na kadhalika, wakaenda kombo, nao wakaingia katika ushupavu wa dini. Ndipo basi ulimwengu mzima, ibilisi anawaelekezea kidole, "Waangalie wale? Waangalie wale?"

Vema, hebu nisimame asubuhi ya leo na nirejee kwenye hawa makumi ya mamiloni mara nyingi ambao hata hawakuanza safari. Vipii kuhusu wao? Mnaona, angalia hali yao. Mwangalie jamaa kama Eichmann leo, akiwa na ya juu kuliko wote ... Wao husema, "Wapentekoste hawana maadili na ni washenzi, wala hawana elimu," na kadhalika namna hiyo. Mwangalieni Eichmann, mmoja wa watu walio na elimu sana ulimwenguni. Naye aliwaua, watoto na wanawake na wanaume milioni sita, nafsi milioni sita. Hutaki kumwelekezea kidole mtu kama huyo.

51 Lakini maskini mtu mdogo ambaye asingeweza kusoma, ilikuwa ni vigumu kwake, labda alilitamka jina fulani la Biblia vibaya, na, ama labda alisema kitu fulani ama akafanya kitu fulani vibaya, ama akafanya kosa fulani, magazeti yanataka kuliandika kila mahali, na kusema, "Si wa kuaminiwa."

Basi ikiwa hao hawawezi kuaminika, kwa nini si elimu, hayo mambo na wenye akili walio nao leo hii? Mwangalie Adolf Hitler. Waangalie wenye akili wa ulimwengu leo hii. Waangalie. Ule msemu wa kale, "Sheria ni msumeno."

Jambo unalopaswa kufanya ni kuweza, kwa Roho Mtakatifu, kutenganisha kilicho kweli na uongo, na kuchukua kilicho ukweli na uongo.

52 Sasa, tunaona ya kwamba Kalvari hii waliyokuwa nayo, nayo maji ya uzima yakawabubujikia watu ...

Sasa, watu wengine wanalo mioyoni na niani mwao, ya kwamba Israeli wote walikunywa, kisha wakawapakia ngamia na kuwafungia farasi wao matandiko, na kadhalika, na kuwachukua watoto wao na kusafiri wakaenda mahali pengine, na kuuacha ule Mwamba pale, ukinyunyiza. Hilo ni kosa.

Huo Mwamba uliwafuata, na hayo maji yaliwafuata. Sasa katika Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 10, ninaamini, na kifungu cha 11, mnaweza kupapata, kwamba, "Mwamba huo uliwafuata Israeli." Popote walipokwenda tangu siku hiyo na kuendelea, Mwamba huo ulienda pamoja nao, nayo maji hayo yakawafuata.

53 Ni mfano mzuri jinsi gani, na ngo—ngome nzuri na nanga kwa mwaminio leo hii, anayejua ya kwamba Mwamba huo ambao ulipigwa wakati mmoja, yale Maji ambayo wakati mmoja yalimwagwa kutoka Kalvari, yanaambatana nasi popote tulipo. Loo, jamani. Siyo kurudi mahali fulani, na kusema, "Vema, kweli tulikuwa na Maji juzi, pale." Tuna Maji leo papa hapa, kwa sababu Mwamba huo ulikuwa ni Kristo. Na Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

Mnaona, Mwamba huo uliwafuata Israeli. Wao kamwe hawakuufuata ule Mwamba, bali Mwamba huo uliwafuata. Amina. Israeli waliendelea na safari yao. Walikuwa na jambo moja tu la kufanya, hilo ni kushika njia iliyonyooka, moja kwa moja kuingia katika nchi ya ahadi. Mwamba huo na maji hayo yakawafuata.

... ule Mwamba ukiwafuata ...

Wakorintho wa Kwanza hukwambia hivyo, mlango wa 10. Vema.

...Mwamba ule ulikuwa ni Kristo

54 Mungu alizichukua hukumu za watu na kuziweka juu ya Kristo, na kumpiga. Je! mliona, kulikuwako na ufa kwenye Mwamba huo, tangu hapo na kuendelea? Mwamba huo ulikuwa na ufa ndani yake, mahali ambapo Musa aliupiga. Naye Kristo alikuwa na ufa wakati alipopigwa, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Kutoka kwenye Uzima huo kunatokea Maji ya Uzima ambayo tunayafurahia sana siku hizi.

55 Sasa, kusudi upate Uzima huu ... Kumbuka, Uzima wa Kristo hudumu na kanisa. Haleluya. Loo, kama tungeweza kutia nanga mawazo yetu pale kwa dakika kumi zifuatazo ... Kristo haliachi kanisa. "Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari." Watu ndio humwacha Kristo, siyo Kristo kuwaacha watu. Watu wanaliacha kwa kutokuamini kwao. Wanamwacha Kristo, siyo Kristo akiwaacha watu.

Israeli walikiacha kijito, siyo kijito kuwaacha Israeli. Mnaona? Kwa kuwa, Biblia inasema dhahiri ya kwamba, "Mwamba ule na maji yale yaliwafuata Israeli: Yaliwafuata. Popote walipoenda, ulienda, pia.

56 Loo, ningetaka, asubuhi ya leo, kama tungelikuwa na wakati, kufungua mlango wa kwanza wa Yoshua, ambapo Yeye alisema, "Kila mahali nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga, nimewapa ninyi. Kila uendako, Bwana, Mungu wako, yu pamoja nawe. Usiogope mtu yeyote. Uwe hodari. Popote tu unapokanyaga, niko papo hapo pamoja nawe, hata iwe ni wapi." Mungu akiambatana na Yoshua ...

Mungu yeye yule anaambatana na kanisa Lake asubuhi ya leo ambapo wanakunywa kutoka kwenye Chemchemi hii huko ng'ambo. Popote utakapokanyaga, hapo ndipo Mungu atakapokuwa pamoja na wewe, kukutia maji na kukupa Uzima. "Nitakuwa pamoja nawe daima, hata ukamilifu wa dahari." Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Sheria za Mungu ...

57 Sasa mnasema, "Basi, Ndugu Branham, ni kwa nini basi hatuyafanyi mambo tunayopaswa kuyafanya? Inakuwaje karama zetu na kadhalika kanisani hazinawiri, kufikia mahali zinapopaswa kuwa? Inakuwaje kanisa letu haliinuki kufikia mahali linapopaswa kuwa?" Watu, kwenye wakati wa majaribu, huanguka kama Israeli walivyofanya. Wanafikiri ya kwamba Mungu amewaacha.

Lakini kumbuka, Mwamba huo kamwe haukuwaacha Israeli. Israeli waliuacha ule Mwamba, walisahau kuhusu ule Mwamba kuwa pamoja nao wakati wote. Ulikuwa moja kwa moja pale, ulitembea moja kwa moja pamoja nao hadi mwisho wa safari. "Uliwafuata." Haukuwa kwenye umbali usioweza kunenewa. Haukuwa kwenye umbali usioweza kusikika. Ama, haukuwa kwenye umbali usioweza kuonekana. Na wala Kristo hayuko pamoja na Kanisa leo; Yeye hayuko kwenye umbali asioweza kuzungumziwa.

Baadhi yenu mmerudi nyuma, na kufanya lile lisilofaa, nanyi mmeipoteza ile furaha, nayo Maji yenu yamekauka. Yeye angali kwenye umbali anaoweza kuzungumziwa kutoka kwako. Yeye huambatana nawe. Anajua kila hatua unayochukua na kila kitu ufanyacho. Yeye ana hamu ya kukusikia ukimwita aje jukwaani.

58 Na huduma hii kubwa ya kipentekoste leo, Mungu anawangojea mumwite jukwaani. Hamko umbali asioweza kuzungumziwa nanyi. Ingawa tumekosea, na kutenda dhambi, na kumpa kisogo, na—na kufanya mambo tusiyopaswa kufanya, lakini hata hivyo Yeye yuko pamoja nasi. Kristo alisema angekuwa pamoja nasi.

Biblia ilisema, "Maji hayo yaliwafuata wana wa Israeli." Waliposhikwa na kiu, walijua maji hayo yalikuwa karibu.

59 Sasa, mambo haya yanadhibitiwa na kanuni. Mfumo wote wa Mungu umewekwa kwa kanuni. Sasa tutachukua... Hebu tusimame kwa dakika moja.

Hebu na tuuchukue ulimwengu. Unazunguka, kila saa ishirini na nne unafanya mzunguko mkamilifu, kamilifu kabisa, huo, kamwe hatujaweza, pamoja na sayansi yetu yote, kuunda saa ya kudumisha majira kikamilifu. Kila baada ya kitambo kidogo, saa zilizo bora kuliko zote walizowahi kuunda, katika mzunguko wa mwaka mmoja, zitaongeza ama kupoteza dakika nyingi. Bali ulimwengu haushindwi kamwe ila uko pale hasa kwenye sekunde. Ni mkamilifu sana hata wanasayansi leo, mamajusi wanaweza kukwambia, katika miaka ishirini tangu sasa ama miaka hamsini tangu sasa, vile hasa jua na mwezi zitakavyopishana. Wakati linapozunguka duara lake la saa ishirini na nne, na kugeuza wakati wake kuzunguka mzingo wake kwa majira, halikosei hata pigo moja. Haleluya. Ni kamilifu, kwa sababu linaenda kulingana na kanuni ya Mungu.

60 Wanajua ni lini hasa hayo maji yatakupwa, kufikia barabara kwenye dakika, kwa kuwa wanajua ni wakati gani mwezi unaposhuka. Naye Mungu ameweka kila kitu kwenye utaratibu kwa kanuni fulani. Na wakati mwezi huo unaposhuka, maji yanakupwa pamoja nao. Mwezi huo unapotokeza, maji hapa yanajaa pamoja nao. Nao wanajua hakika, kwa kupima wakati, wakati mwezi huo utakaposhuka. Wanaweza kuiweka kwenye kalenda ya shajara kwa miaka kadhaa kabla, na kuwaambia, mpaka dakika, wakati maji hayo yatakapoanza kupwa. Hakika, kwa kuwa hivyo ndivyo mwezi unavyoondoka, kwa sababu umewekwa katika utaratibu wa kanuni za Mungu.

61 Nilikuwa nimesimama hivi majuzi karibu na Ziwa Michigan. Ndipo nikaenda kwenye Ziwa Superior, nikienda zangu Canada, huo mtandao mkubwa mno wa maji. Nami nikasimama pale, na nikawaza, "Ni maili ngapi kuyavuka maji haya sambamba hapa?" Na halafu baada ya mimi kuvuka Michigan—ama Ziwa Superior, ningeingia ndani ya Michigan, karibu mkusanyiko sawa wa maji. Na kwenda kule, kutoka Ziwa Superior hadi Ziwa Michigan, kutoka Ziwa Michigan hadi Ziwa Ontario, na ninii tu—na Huron, na maziwa yote pamoja. Ni mabilioni mangapi mara mabilioni mara mabilioni, na matangi yasiyohesabika ya maji safi yaliyo kwenye ziwa hilo.

Na huko Nevada, na katika Arizona, New Mexico, California Mashariki, kuna mamilioni ya ekari za mashamba yaliyokauka, yanayoungua, ambayo yana rutuba sana kiasi kwamba, kama maji hayo yangeweza kufika kwenye ardhi hiyo, taifa hili lingeweza kuulisha ulimwengu, pasiwepo watu wowote wenye njaa, na wawe na mabaki ya kutupa baharini. Hiyo ni kweli. Yale mamilioni ya ekari ambazo zingekuza tani mara mamilioni ya tani za viazi, na kabichi, na maharagwe, na—na saladi, na figili na seleri, na matango, na kadhalika. Ardhi hiyo ingezikuza, ina—inatamani tu ipate maji.

62 Na haya hapa maji *hapa* juu, na huu hapa udongo *hapa* chini. Sasa tunaweza kuyaona, na tunajua yangefanya hivyo, kwa kuwa tunaweza kuyafanyia maji hayo uchunguzi na kuona ni safi, na kuufanyia udongo uchunguzi na kuona una rutuba. Sasa, shauku yote tunayoweza kuwa nayo, kamwe haitayaleta pamoja. Lakini, kuna kanuni, na kanuni hiyo ni kanuni ya uvutano. Sasa, kama tukifuata kanuni ya uvutano, tungeweza kunyunyizia kila sehemu ya ardhi hiyo, tukiyatoa maji kwenye maziwa hayo na kuyamwagilia. Lakini itatubidi kufanya kazi kulingana na sheria ya uvutano. Hatuwezi kuwa na shauku hata yakatoka kule. Hatuwezi kuyapigia yowe hata yakatoka kule. Hatuwezi kuyapigia kelele hata yakatoka kule. Inatubidi kufanya kazi kulingana na kanuni za uvutano, kuyapeleka kule. Mungu huweka kila kitu katika kanuni.

63 Hapa, nilikuwa nikiwazia, sijui kama nilipata kuwaambia jambo hili, au la. Nilikuwa huko chini Kentucky, nikiwinda kuchakuro, pamoja na Ndugu Wood, yapata mwaka mmoja uliopita. Nasi tunaninii ... Kuchakuro kwa namna fulani walikuwa ni adimu, na kwa hiyo tukaenda nyumbani kwa jamaa fulani, kutafuta habari za kuwinda. Mtu fulani alikuwa na shamba la ekari kadhaa, na kwenye shamba hili kulikuwako na msitu mkubwa. Lakini Ndugu Wood akaniambia ya kwamba mtu huyo ni kafiri. Yeye—yeye ni asiyeamini. Kwa hiyo alisema ya kwamba alimfahamu, kwa hiyo yeye—ama baba yake alimfahamu, angeenda kule amwombe kama tungepata ruhusa ya kwenda kuwinda.

Tukaenda kwa gari hata nyumbani kwa mwungwana huyo. Na yeye na mtu mwingine, wote wawili wakiwa na umri wa miaka sabini, walikuwa wameketi chini ya mtofaa. Basi Bw. Wood akamwendea mtu huyu, na akamwambia, "Naweza kuwinda kidogo huku kwako?" Naye akasema, "Vema," akasema, "sawa." Akasema, "Wewe ni Wood yupi? Wewe ni mvulana wa Jim Wood?"

Akasema, "ndiyo."

Akasema, "Vema, mzee Jim alikuwa ni mtu mnyofu, na kadhalika." Akasema, "Unaweza kuwinda popote utakapo, shambani mwangu. Nina ekari mia kadhaa hapa; jitudumie. Shuka uende mabondeni, popote utakapo. Jisikie tu nyumbani."

Niliketi kwenye gari, kwa kuwa nilidhani mhubiri na kafiri hawataendana vizuri pamoja, kama tulikuwa tunaenda kuomba fadhili za kafiri.

64 Kwa hiyo basi baada ya kitambo kidogo, Ndugu Wood akasema, "Vema, sasa, naweza kwenda pamoja na mchungaji wangu? Nafikiri ingekuwa ni sawa kwake kuja."

Ndipo mzee huyu akageuka kwa fimbo yake, na akasema, "Wood, unataka kuniambia ya kwamba umejishusha sana, hata inakubidi kuwa na mhubiri kokote uendako?"

Na kwa hiyo, nikawazia, baada ya hayo, ni afadhali nitoke kwenye gari. Kwa hiyo nikatoka kwenye gari, na nikazungumza na mzee huyo mwungwana kwa dakika chache. Naye akanijulisha upesi sana ya kwamba hakuwa na haja sana na wahubiri, kwa sababu alidhani walikuwa wakizungumzia kitu ambacho hawakujua kitu juu yake.

Akasema, "Wanafokea tu kitu wasichojuu lolote kukihusu. Vema," akasema, "mtu anapozungumza nami, ninamtaka ajue analozungumzia." Sasa, hiyo ni hekima nzuri. Sasa, hiyo ni hekima nzuri. Akasema, "Sasa, kama mtu akizungumza nami, sitaki azungumzie kitu fulani, kinginecho, cha kudhania ambacho hajui chochote kukihusu. Ninamtaka azungumzie jambo ambalo anajua anachozungumzia." Vema, niliheshimu hilo. Niliheshimu hilo katika mzee huyo mwungwana.

Na kwa hiyo nikasema, "Vema, hakika, hiyo ni kila mtu na maoni yake."

65 Naye akasema, "Kulikuwako na mhubiri mmoja aliyekuja hapa nchini miaka michache iliyopita, ambaye alikuwa na mkutano kule Acton." Kisha akasema, "Huyu mhubiri, usiku mmoja, akiwa ni mgeni humu nchini, alimwambia ma—mama mmoja aliyekuja ameketi kwenye wasikilizaji, 'Una lesu mfukoni mwako. Nawe ni Bibi Fulani. Nawe una dada aliye mgonjwa juu ya kilima hapa. Jina lake ni *Fulani*. Anakufa kwa saratani tumboni.' Kisha akasema, 'Chukua lesu hii na uiweke juu ya dada yako, na umwambie,' BWANA ASEMA HIVI," hatakufa, bali ataishi."

Akasema, "Mwanamke huyu huyu alikuwa rafiki yetu." Kisha akasema, "Tulimchukua mwanamke huyu ... Lesu hii huko juu; ama mtu huyu, kwa mtu huyu ..." Kwanza alisema, "Huyu mwanamke, mimi pamoja na mke wangu tulikuwa huko juu asubuhi hiyo na tulikuwa tumechukua, tukamhudumia huyu mwanamke. Naye alikuwa hawezi kabisa madaktari walikuwa wamemkatia tamaa, muda mrefu uliopita. Alikuwa mnyonge sana hata ilitubidi tumbembe kwa shuka, kumwinua kumweka kwenye chombo cha kujisaidia kitandani mwake, kisha kumrudisha. Kumgeuza kwenye shuka, alikuwa ni dhaifu sana." Akasema, "Usiku mmoja, huko, kulitokea kelele kana kwamba walikuwa na mtu aliyekufa."

66 Huyo alikuwa ni Ben huko, akiwa na lesu hiyo, akiipeleka pale. Ninaamini ilikuwa ni wewe, sivyo, Ben? [Ndugu Ben anasema, "Amina. Amina." - Mh.] Ilikuwa ni Ndugu Ben pale, akichukua lesu hiyo, maana alimchukua mwanamke huyo kule.

Kisha akasema, "Kesho yake asubuhi alikuwa akila mikate ya tofaa." Na akasema, "Yeye hafanyi kazi yake tu, bali anafanya kazi ya jirani. Alikuwa mzima sana. Akasema, "Sasa, mara nyingi nimeshangaa. Kama nikipata kumwona mhubiri huyo, yeye alijua alilokuwa akizungumzia," kasema, "Ni—ningetaka kuzungumza naye."

Ndugu Wood akaniangalia, nami nikamwangalia. Nimesimama pale, mchafu, na nimejaa jasho na ni mchafu, tulikuwa tumepiga kambi msituni, na—na damu ya kuchakuro imetutapakaa kote. Na kwa hiyo nikasema, "Vema," nikasema, ni ... Unamaanisha ya kwamba ungeweza kuzungumza na jamaa huyu naye angekuambia jinsi alivyofanya jambo hilo?

Akasema, "Naam, bwana, hivyo ndivyo ninavyomaanisha."

Nikasema, "Vema, hilo—hilo ni jambo zuri."

67 Nilikuwa nikila moja ya matofaa yake. Maskini nyigu wadogo walikuwa wakiyavamia, mwajua, kwenye msimu wa mwaka wa majani kupukutika, Agosti. Kwa hiyo nilikuwa na tofaa hili dogo, nami nilikuwa nimeligh'ata kidogo. Nami nikasema, "Hilo ni tofaa nzuri sana." Nikasema, "Mti huo umekuwa pale kwa muda gani?"

"Loo," akasema, "niliupanda huo mti kule, miaka thelathini ama arobaini iliyopita, ama kitu kama hicho."

"Naam, bwana." Nikasema, "Ningetaka tu kukuuliza swali." Nikasema, "Vipi ulimwenguni ... Ninaona hayo matofaa yameanguka kutoka kwenye mti huo, na majani yake yanapukutika, na hapa ni katikati tu ya Agosti." Nami nikasema, "Hata hatujapata kuwa na baridi; hata hatujapata baridi wala cho chote kile, na hata hivyo majani hayo yanapukutika kutoka kwenye mti huo. Mbona hivyo?" Yeye alisema, "Utomvu umeuacha mti." "Loo," nikasema, "ulienda wapi?" Yeye alisema, "Huko chini kwenye mizizi." Nami nikasema, "Basi utakaa muda gani huko chini?" Akasema, "Mpaka majira ya kuchipua."

Nami nikasema, "Basi utapanda juu tena, na kuwaletea majani mapya kwa ajili ya kivuli, matofaa mapya ya kula." Akasema, "Hiyo ni kweli. Sawa kabisa."

68 Nikasema, "Vema, nataka kukuuliza jambo fulani, bwana. Unazungumza juu ya jamaa hawa ambao hawajui wanalozungumzia." Nikasema, "Je! ungeweza kunielezea ni Akili gani inayoufanya huo utomvu kuondoka kwenye mti huo? Kama ungalikaa mle kote katika majira ya baridi kali, huo mti ungekufa. Ungeuua mti huo. Chembe ya uhai iko kwenye utomvu huo." Kwa hiyo nikasema, "Ungeuua mti huo. Ni Akili gani inayoufanya huo utomvu kuondoka kwenye huo mti, ukaingia mizizini, na kukaa mpaka kwenye majira ya kuchipua, na kisha upande juu tena na kuzaa matofaa zaidi?" Nikasema, "Tia maji kwenye ndoo na uiweke kwenye mlingoti, na uone kama, kwenye Agosti, yatateremka chini ya huo mlingoti na kurudi kwenye majira ya kuchipua Mnaona? Nikasema, "Kuna kanuni fulani, kuna kanuni ya maumbile. Akili fulani iliweka kanuni hii katika utaratibu. Siyo hivyo tu, bali Akili hiyo hiyo haina budi kutekeleza hizo kanuni, ambazo huusukuma chini kwenye mizizi ya mti huo, kisha ukarudi."

Akasema, "Kamwe sikuwa nimeliwazia hilo."

Nikasema, "Waweza ... Kama ungaliweza kujua Akili hiyo inayoufanya huo utomvu kutoka kwenye matawi ya huo mti, ukaingia kwenye mizizi na kurudi, hiyo ndiyo Akili ile ile iliyoniambia huko usiku ule, 'Nenda, ukaiweke lesa hiyo juu ya mwanamke huyo.'" Akasema, "Na wewe ndiwe yule mhubiri?" Nikasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli."

69 Mwaka uliopita nilikuwa huko (yeye ameshaondoka), na mjane wake alipokuwa ameketi barazani, akimenya matofaa, kutoka kwenye mti uo huo. Ndugu ... Kwanza walikuwa watufukuze, hawakujua tulikuwa ni akina nani. Nami nikaenda na kumwambia kuhusu hilo, ya kwamba tulikuwa na ruhusa ya kutoka kwa mumewe. Na nikamwambia hivyo, kasema, "Yeye alimkiri Kristo kikamilifu kabla hajafa."

Mnaona, ni kitu gani kinachoufanya huo mti, ni Akili gani inayousukuma huo chini? Ni kanuni. Ni kanuni ambayo Mungu ameiweka katika utaratibu. Na kanuni hiyo ni kanuni ya Mungu ambayo italishughulikia jambo husika. Amina.

Unajua, sijali jinsi gani, unapiga makelele kiasi gani, na kusema—kusema sasa, "Haita ... Jua halitaangaza tena msimu huu wa kiangazi." Litaangaza, kwa vyovyote. Ni kiasi gani utasema, "Si—si—sitauruhusu usiku uje." Utakuja, kwa vyovyote. Kwa sababu kitu hiki tunachoishi juu yake, kinachoitwa ulimwengu, kimedhibitiwa na kanuni ya Mungu.

70 Sasa, ndugu na dada, ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Basi kama tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu ... Mungu hana sehemu ndogo zilizo dhaifu na sehemu kubwa zenye nguvu; Yeye ni Mungu kabisa! Na kama ulikuwa na kiasi cha Mungu cha kutosha ndani yako, mpaka ilikuwa angalau tu ni kivuli, hizo ni nguvu za kutosha kuumba dunia mpya. Hizo ni nguvu za kutosha kufanya mwezi mpya na mfumo mpya. Ni Mungu, na ina nguvu! Na sasa hivi kila mwaminio hapa ndani yuna Uzima wa Milele, ambao ni, Roho wa Mungu ndani yako; Nguvu za kutosha zitakazowafufua wafu, zitakazowaponya wagonjwa, zitakazoiweka mizingo katika hali nzuri. Lakini unaninii ... Unaongozwa na kanuni fulani, Roho huyo aliye ndani yako. Ninyi ni wana na binti za Mungu. Roho yule yule uliye naye ndani yako, atajifufua mwenyewe katika siku ya ufufuo.

71 Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, wakati alipokufa, nafsi Yake ilishuka Kuzimuni, na akawahubiri roho waliokuwa kifungoni, nafsi zilizokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu. Mwili wake uliingia kaburini. Lakini kabla hajafa, alimkabidhi Roho Wake mikononi mwa Mungu. Roho Wake alimwendea Mungu; Nafsi yake ilienda kuzimu; na mwili Wake ukaenda kaburini. Naye Yesu alizuiliwa asifufuke mpaka Maandiko yaweze kutimia. Asingeweza kurudi, kwa sababu ilimbidi kukaa kaburini siku tatu usiku na mchana. Lakini wakati Maandiko yote yalipotimizwa, kizuizi hiki kiliondolewa; Roho Yake ikashuka kwenye nafsi Yake, nafsi Yake kwenye mwili Wake, Naye akafufuka tena.

72 Nasi tunapokufa, nafsi zetu zitaenda chini ya madhabahu ya Mungu; ambapo nilipewa majaliwa ya kupaona, asubuhi chache zilizopita, kama mjuavyo, katika ono, ambapo Biblia inazungumza habari zake. Roho zetu zitaenda kwa Mungu aliyezitoa, na miili yetu itarudi kwenye mavumbi ya ardhi. Lakini siku moja, wakati Maandiko yatakapotimizwa, roho zetu zitaachiliwa kutoka kwa Mungu, zitaichukua nafsi, nayo nafsi iuendee mwili. Na nguvu zitakazotufufua, zimo ndani yetu sasa. Sasa tuko katika ulimwengu wa roho. Sasa tuko katika nguvu za ufufuo.

Kama kusingekuwako na kanuni zake, wana na binti za Mungu wangelijumbia ulimwengu hapa na waende wakaishi maisha ya peke yao kwenye huo. Una nguvu ndani yako ya kufanya jambo hilo. Kama una kivuli cha Nguvu za Mungu ndani yako, una Nguvu za kufanya hivyo. Mungu ni muweza wa yote. Mnaona ninalomaanisha? Nguvu zilizo ndani yako zitafanya ... Ungeweza kuunena ulimwengu ukaweko na uende ukaishi humo. Haleluya. Haya basi.

Hizo ndizo Nguvu zilizomo Kanisani sasa, bali zinadhitiwa na kanuni fulani. Na hiyo kanuni si "kushika lundo la amri." Ni kanuni ya imani. Yesu alisema, "Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Na kama unaweza kuliadini, chochote kile Mungu ataiongoza nafsi yako kuamini, hicho ni chako. Kila mahali nyayo za miguu yako zinapoweza kukanyaga, kwa imani, Mungu anakupa wewe. Amina. Ni pako, unapamiliki, ikiwa unaweza kupata ufunguo wa hii kanuni ya imani inayokufungulia huo. Mnaona

ninalomaanisha? Nguvu hizo zinatawaliwa na ... Ikiwa wewe ni mwana wa Mungu, wewe ni binti ya Mungu, hizo hazikuachi. Ziko pamoja nawe wakati wote. Lakini, imani yako huziacha, bali zingalipo. Haleluya.

73 Wakati unapookolewa, Mungu hukupa imani kuinuka kutoka kwenye kinyaa cha dunia. Imani yako inashinda mambo ya ulimwengu. Imani yako ni nini? Imani yako ni lile tendo ambalo Mungu amefanya ndani yako kukufanya mwana wa Mungu. Unaacha kusema uongo kwako, unaacha kuiba kwako, unaacha kunywa pombe kwako, kwa sababu imani yako inakuinua juu yake. Amina. Usipofanya hivyo, huna imani yo yote. "Na kwa imani mmeokolewa, na kwa neema."

Kadiri ya imani yako itakayoachiliwa, hicho ndicho kiasi cha Nguvu unazoweza kuwa nazo, kwa kuwa ndani yako mnaishi Nguvu za kufanya Mbingu na nchi. Mungu anaishi ndani yenu, nanyi ni wana na binti za Mungu. Amina. Haya basi. Lakini ni imani yako. Yesu alisema, "Kulingana na imani yako, na iwe kwako. Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana. Amin, nawaambia, ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitilie shaka, bali uamini yale uliyosema ..."

74 Basi tunapaswa kuwa watu, wa namna gani, tukiwa na imani katika huyu Kristo mkuu anayekomboa anayeishi ndani yetu, Mwamba huu uliopigwa ambao hauliachi Kanisa? "Niko pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari," Uwepo udumuo daima wa Kisima hiki kikuu kinachobubujika cha wokovu na Nguvu zilizomiminwa kutoka Kalvari hadi Kanisani, Uwepo udumuo daima wa Mungu aliye hai, Mwamba mkuu uliopigwa, unaobubujika na kuambatana nasi katika safari yetu.

75 Israeli walipoteza imani yao. Waliondoka njiani. Walianza kutamani sufuria za nyama. Kama wangelidumu na imani, na wakiamini ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kuwapeleka kwenye nchi ile, kusingekuwako na chochote kingaliwazua. Walikuwa tayari wamezifungua bahari, walikuwa wameleta mapigo juu ya adui zao, walikuwa wamewasulibisha adui zao nyuma yao, na walikuwa wameenda wakaingia kwenye nchi ile, na bado wasingekuwa na imani ya kutosha kuingia kwenye ahadi ile.

Yoshua na Kalebali walikuwa na imani hiyo. Walisema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kushinda chochote ambacho kingekuja mbele zetu."

Hiyo ndiyo shida ya kanisa. Tunaweza kushinda kila ugonjwa. Tuna nguvu ndani yetu. Sisi ni wana na binti za Mungu, hakuna kitu kinachoweza kusimama mbele zetu. Jambo la pekee, Yeye anataka kumpata mtu fulani atakayeliadini, ambaye ataamini kile Mungu amewafanyia tayari. Siyo tutakuwa; tuko sasa! Nao Uwepo unaishi daima wa Roho uko pamoja nasi. Amina. Haya basi.

76 Hilo ndilo nililomaanisha wakati nilipozungumzia somo hilo asubuhi ya leo, *Maji Yaliyopo Daima Yatokayo Mwambani*. Maji yaliyopo daima yatokayo Mwambani yapo hapa sasa, hayo Maji yaliyopo daima yatokayo kwenye Mwamba uliopigwa pale Kalvari. Wakati huyo Roho Mtakatifu alipotoka ndani Yake pale Kalvari, huyo aliyerejea juu ya Kanisa kwenye Siku ya Pentekoste, Roho Mtakatifu yuyo huyo yupo asubuhi ya leo. Naye ametupa ahadi!

Hiyo ndiyo sababu, nilipotembea mbele ya wagonjwa, wakati Yeye aliponiagiza huko ng'ambo, ninaliamini; Mungu alisema hivyo. Hivyo ndivyo maono hutukia; Mungu aliliahidi. Mungu hawezi kusema uongo.

77 Aminini. Huna budi kuamini hilo. Hapana budi pawe na kitu pale, fungua valvu hiyo, fungua kitu hicho kikuwezeshe kuingia ndani yake. Tunachohitaji leo hii si kuomba tupate Nguvu nyingi zaidi. Una nguvu za kutosha kuifanya dunia mpya. Unachohitaji ni imani kutumia nguvu hizo. Unachohitaji ni kuyadhibiti hayo maisha, na kuishi maisha ya kitauwa sana, hata unapomwomba Mungu chochote, mnajua. Tuna imani na Mungu, juu ya jambo hilo. Tunajua, kama tukitii amri Zake, Yeye hatatunyima kitu chochote chema, kama tukitembea na Yeye. Mungu akitembea pamoja nasi. Loo, jamani.

78 Walikuwa na jambo moja tu la kufanya. Walikuwa na jambo moja tu la kufanya; wale ambao wanakaa moja kwa moja njiani, si kuzurura *huku*, na kutangatanga *kule*, bali kudumu moja kwa moja safarini. Kanisa lina jambo moja tu la kufanya: kudumu safarini. Walikuwa na Nguzo ya Moto, waliyokuwa nayo, ya kujidumisha safarini kwa: kuifuata hiyo Nguzo ya Moto. Hilo ndilo lililowaongoza. Kitu chao walichoweza kuona, kilikuwa ni ile Nguzo ya Moto. Waliiona ikitenda kazi kupitia Musa, nao wakajua ya kwamba yeye alikuwa ndiye kiongozi.

Leo tuna Neno. Tunalifuata Neno. Nasi tunaona Neno likitenda kazi ndani ya waaminio, nasi tunajua ndivyo ilivyo basi: Mungu akitenda kazi pamoja nasi, akithibitisha Neno kwa ishara zinazofuata. Tunadumu na Neno. Neno hutoa matokeo.

Walikaa pamoja na—na Musa. Kwa sababu ile Nguzo ya Moto, Musa aliifuata Hiyo. Nao wakafuata. Walipoanza kugeuka dhidi ya Musa, na kunung'unika dhidi ya Mungu na dhidi ya Musa, walianza kutangatanga upande mmoja na mwingine. Taabu zikaingia. Hakika.

79 Tunadumu na Neno, nalo Neno hutoa ishara. Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao

wanaoliamini Neno." Mnaona, linakaa pamoja na... Ukidumu na Neno, Neno linazaa ishara. Lakini Musa, alifanya nini?

Walitangatanga, nao walifanya nini? Waliacha njia, ndipo wakapoteza ruzuku yao ya maji.

Nafikiri hilo ndilo kanisa limefanya leo hii. Limeondoka kwenye njia ya Maandiko. Wameingia kwenye itikadi. Wameingia kwenye mambo madogo ambayo hawapaswi kufanya. Walichukua mambo. Walichukua mambo kama Imani ya Mitume. Unapata wapi hilo katika Biblia? Walichukua katekismu waliyosoma. Walichukua madhehebu badala ya tukio. Walichukua kupeana mikono badala ya tukio la kuzaliwa mara ya pili. Walichukua kunyunyizia badala ya ubatizo wa maji. Walichukua mfano mbaya, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," wakati hakuna kitu kama hicho katika Biblia. Biblia ilisema, "Katika Jina la Yesu Kristo." Kuna jambo moja tu la kufanya kama unataka Maji yale yale, rudi kwenye njia tena. Rudini kwenye ... Hajaondoka; Yeye yungali hapa.

80 Unachukua kanuni za imani badala ya Kristo. Unatangatanga kwa hasira. Mmoja alisema, "Vema, mimi ni Mmethodisti." Mwingine anasema, "Mimi ni Mbatisti." Hiyo inaonesha ya kwamba wewe si Mkristo wakati huo. Sisi ni wa Kristo. Sisi ni mali Yake. Unasema, "Vema, kama mimi, Mbaptisti." Kama hivyo ndivyo ulivyo tu, basi wewe si wa Kristo; wewe ni Mbatisti. Unasema, "Vema, mimi ni Mpentekoste." Kama wewe ni Mpentekoste tu kwa dhehebu, hivyo tu ndivyo ulivyo.

Lakini kama una ujuzi wa Kipentekoste ... Nalo Neno la Kipentekoste litazaa tukio la Kipentekoste. Fuata jambo lile lile wanafunzi hao walilofanya; kaa kule juu mpaka utakapojazwa na Roho Mtakatifu. Na halafu kama ukipata kinyume cha Neno, roho huyo aliye ndani yako huenda kinyume na yale Neno lisemayo, basi si Roho Mtakatifu. Ni ibilisi akimwiga Roho Mtakatifu. Mnaona mahali tulipofikia?

81 Loo, baadhi yetu walinena kwa lugha, tulikuwa na vipindi vya kupiga makelele na kadhalika namna hiyo, na kukana mambo haya mengine yote. Tuliruhusu kila kitu ambacho hakikuwa katika Maandiko kuja kanisani. Tumefikia wapi leo? Tumerudi kwenye jangwa lingine, dhehebu lililokauka. Tuliunda madhehebu; tulipoteza Maji yetu. Hivyo ndivyo Pentekoste ilivyofanya hasa. Wakati ilipoanza kujiundia madhehebu, ilianza kuvunja ushirika, na kusema, "Vema, sasa hatutashirikiana, kama jamaa huyu anaamini *hilo*."

Endeleeni, dumuni pamoja naye mpaka atakapofikia Neno la Kweli, ujuzi wa Kweli. Chochote kile, kiacheni, hata hivyo. Endeleeni tu, iweni kama ndugu.

Lakini, loo, ilitubidi kujiundia dhehebu, na kusema, "Vema, kwa kuwa wewe si wa Umoja, kwa kuwa wewe si wa Uwili, ama wa Utatu, ama namna hii, hatutakuwa na ushirika na wewe." Ndipo tunapofanya jambo hilo, tunafanya nini? Tunajirudisha moja kwa moja jangwani tena. Hiyo ni kweli.

Lakini kumbuka, wakati Israeli walipotangatanga kutoka kwenye njia, njia ya kwenda kwenye nchi ya ahadi, Mwamba haukuwaacha; Ulikaa papo hapo; vivyo hivyo na maji. Vivyo hivyo na Roho Mtakatifu, anakaa papo hapo. Haitubidi kurudi nyuma.

82 Sasa, hapa Mungu anatumfundisha jambo kuu. Mungu hutufundisha hapa somo. Kristo alipigwa mara moja, akitupa tukio la Kipentekoste wakati mmoja kwa wote. Sasa, wakati Mwamba huo ulipopigwa, haikupaswa kupigwa tena. Ulipigwa mara moja tu.

Musa alifanya kosa kwa kuupiga mara ya pili, akionesha udhaifu wa imani yake katika Upatanisho. Lakini wakati Kristo alipopigwa mara moja, haimbidi kamwe kupigwa tena. Vema, Musa alikuwa akifanya nini? Musa alikuwa akianzisha kitu kipya, akijaribu kufanya jambo jipya.

Na hivyo ndivyo makasisi wetu wamefanya leo. Wamejaribu kufanya kitu kipya. "Tutajifanyia wenyewe Assemblies of God. Tutajifanyia Kanisa la Mungu la Kipentekoste. Tutajifanyia Baraza Kuu. Tutajifanyia *hivi, vile, ama vinginevyo*." Hivyo sivyo Mungu alivyofanya. Hilo halikuwa wazo Lake.

83 Kristo alipigwa mara moja. Hilo ndilo tukio la asili. Hiyo ndiyo njia ya asili. Katika siku ya Pentekoste, Petro alisema, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo."

"Tunanyunyizia katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, kutoa kila namna ya kanuni za imani na cho chote kile." Tunapoondoka kwenye Neno, si ajabu hatuwezi kufika po pote ...?...

84 Mungu hutufundisha somo. Musa hakupaswa kusema, "Sasa, tutaanzisha kitu kipya hapa sasa, na tutaunda madhehebu, nasi tutaliunda kanisa Katoliki." Hilo ndilo jambo la kwanza walilofanya. La, basi baada ya kitambo kidogo, "Vema, tutaanzisha kitu kipya kutokana na hayo; tutawafanya Walutheri." Ndipo wakaja Waanglikana, na halafu Wabatisti, na kadhalika, na Wakampbeli, na Kanisa la Kristo, na mpinga -Kristo, na mambo mengine yote. Mnaona? Wote wakaanza kwenda, mmoja baada ya mwingine, mmoja baada ya mwingine, wakifanya madhehebu na madhehebu. Haikuwa hivyo. Mnaona pale kile wanachofanya? Wanaupiga Mwamba tena kuanzisha kitu kipya. Hatuhitaji fundisho jipya.

85 Kila mtu katika Biblia alibatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Kila mtu katika Biblia aliye na Roho Mtakatifu akija kwa njia ya Mungu, jinsi hasa Mungu anavyofanya—alivyofanya katika ...?... Walifanya

jambo lile lile. Walikuwa na tukio lile lile. Ishara zile zile ziliwafuata. Kazi zile zile ziliwafuata. Kwa nini? Waliishi karibu na Mwamba. Walipata Maji yale yale.

Na leo, sababu ya sisi kuwa na kanuni nyingi sana za imani na madhehebu, ni kwa sababu tunaanzisha kitu kipya. Hatuhitaji kitu kipya. Rudini nyuma ...

Musa hakupaswa kuupiga ule Mwamba tena, kuanzisha kitu kipya. Alipaswa kuwaambia juu ya ule Mwamba wa asili. Loo, natumaini mnapata jambo hilo. Musa alipaswa kunena juu ya ule Mwamba uliopigwa awali, si kujaribu kuupiga tena, si kujaribu kuanzisha jambo jipya, bali kunena na Kitu hicho cha zamani!

86 Mungu, nisaidie. Kama nikifa ombaomba, mimbarani, nitanena juu ya Mwamba wa asili! Nitazungumza juu ya tukio la asili. Nitanena juu ya Maandiko ya asili yaliyowapa ubatizo wa Roho Mtakatifu, "Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." Uwepo wa daima wa Maji yanayotiririka kutoka kwenye Mwamba ungali uko pamoja nasi. Utaleta jambo lile lile. Utaleta maono. Utaleta uponyaji. Utaleta unabii. Utaleta kila kitu walichofanya.

87 Wakati Israeli walipopanga mstari katika Maandiko tena, na kurudi njiani, walienda kwenye nchi ya ahadi. Lakini iliwachukua miaka arobaini.

Pentekoste imekuwa yapata miaka arobaini ama hamsini, wakizunguka -zunguka jangwani. Rudini kwenye Mwamba. Unaonekana. Hapa imeandikwa papa hapa kwenye Neno. Roho Mtakatifu yuko hapa akitenda jambo lile lile alilofanya daima, kwa hiyo uwepo wa daima wa Maji upo hapa. Rudini tu Kwake, rudini kwa yaliyotangulia, ya asili.

88 Ilikuwa katika ya asili? "Vema, walipeana mikono na mhubiri." Hakuna kitu kama hicho. "Walibatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Hakuna kitu kama hicho. Hakuna watu katika Biblia, mahali popote, au nje, miaka mia tatu nje ya Biblia, waliopata kubatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Hiyo ni kanuni ya imani ya Katoliki, si fundisho la Biblia. Mnaona?

89 Walikuwa na Roho Mtakatifu. Ishara hizi ziliwafuata wale walioamini. Zitafanya hivyo tena leo. Mwamba huo ni wa milele tu kama ulivyowahi kuwa, ule Mwamba uliopigwa.

Hebu tuiseme, "Vema, sasa njoni mkajiunge na kanisa letu la Kipentekoste, ingieni katika milki yetu ya Kipentekoste." "La, unakuja na kujiunga na Baptisti, ama Methodisti, ama Presbiteri, ama Katoliki." Ni kitu gani hicho? Huko ni kuupiga Mwamba tena, kujaribu kuanzisha kitu kipya.

Waambie, "Tubuni, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo," kwa ondoleo la dhambi zao," na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Sasa mmerudi njiani, mmerudi kwenye Maji yale yale. Maji yale yale yatatoa viburudisho vivyo hivyo. Yataupa mwili kusuguliwa kule kule. Yatatoa nguvu zile zile za kuosha. Yatatoa nguvu zile zile za uponyaji. Yatafanya jambo lile lile yaliyofanya wakati ule, kama tutarudi tu kwenye Roho yeye yule.

90 Uhai uliomo kwenye mzabibu utazaa mizabibu. Kama ulizaa mwaka jana, utazaa kitu kile kile mwaka huu. Hiyo ni kanuni ya Mungu. Kanuni ya Mungu ni kwamba, kama huu ni mzabibu, achana nao, utazaa mizabibu. Unaweza kuuzalisha na kitu kingine, bali hata hivyo achana nao nao utarudi kwenye mizabibu ile ile tena.

Kwa hiyo tumelizalisha kanisa na Upentekoste, na Ubaptisti, na Umethodisti, na Upresbiteri, na—na Uanglikana, na kila namna nyingine ya itikadi. Kwa nini msiliache peke yake? Rudini kwenye Mzabibu, utarudi kwenye Nguvu zile zile. Amina. Amina. Ninapenda jambo hilo.

91 "Anzisha kitu kipya." Jambo lile lile ambalo tumelifanya. Siyo kujaribu kuonyesha mamlaka yetu. "Daktari *Fulani* ni mwanzilishi wa kanisa kubwa la *Fulani* la *fulani na fulani*." Kwa hiyo, hilo lilikuwa silo.

Hivyo ndivyo Musa alivyosema, "Nitawaonesha kile ninachoweza kufanya. Nitayaleta, hata hivyo!" Akaupiga, hayakutokea. Akapiga makelele tena, "Nitaonesha kile ninachoweza kufanya." Mungu alikuwa na neno naye kwa ajili ya jambo hilo.

Msifikiri, kama wewe "ukishikilia tu kwenye dhehebu fulani. Mungu atakuwa na neno naye kwa jambo hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Hamna budi kurudi kwenye ile ya asili. Rudini.

92 Nena tu na watu. Usiwaambie, "Ninyi njooni mkajiunge na kanisa letu. Njooni mkaikariri kanuni yetu ya imani." "Rudini mkatubu, na mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu; nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kama moyo wako uko sahihi. Na ishara hizi zitafuatana na waaminio. Kundi la waaminio, ishara hizi zitaambatana nao." Kwa sababu gani? Mwamba, Mwamba uliopigwa na Maji Yake ya Uzima yanatoka moja kwa moja, yakitoa kitu kile kile Yeye alichokitoa kule nyuma. Hayawezi kujizuia.

Loo, naam. Tunataka kujivunia, na kusema, "Sisi ni Wamethodisti na Wabatisti."

93 Nena tu na Mwamba; Yeye yupo daima. Usijaribu kujiunga Nao. Nilikuwa "nimejiunga" hapa chini. Usijaribu kujiunga Nao. Huwezi kujiunga na Huu, hilo ni jambo la hakika. Unaweza kujiunga na Methodisti, unaweza kujiunga na Baptisti, unaweza kujiunga na Wapentekoste, unaweza kujiunga na Waanglikana, lakini huwezi kujiunga na Huu. La. Huna budi kujazwa na Huyu. Usijiunge Nao; jazwa tu Naye. Hivyo tu. Ni kujazwa na nini? Kujazwa na Nguvu, kujazwa na Roho, kujazwa na Uzima, kujazwa na furaha, amani, uvumilivu, upole, wema, Nguvu za Roho Mtakatifu maishani mwako, kwa kuwa Uwepo wa milele umo mle. Kumbukeni.

(Itanibidi kufunga, maana inachelewa.)

94 Lakini, kumbukeni, huo Mwamba kamwe haukuwaacha. Kamwe haukuwaacha. Naye Kristo kamwe hatatuacha; Kristo alisema, "Nitakuwa pamoja nanyi daima, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo ni kweli? Nao huo Mwamba ulikaa pamoja nao kote kote kutoka Horebu hata Nebo. Ulikaa. Mpaka huko Yordani, ulikuwa ungalii pale. Ee Mungu, ninataka kuuona huko Yordani!

Musa, wakati alipokuwa huko Yordani, Mwamba ulikuwa pamoja naye kote njiani. Naye alikuwa amesimama pale juu, akiangalia chini kwenye ku—kundi la watu waliokuwa wamerudi nyuma na kumwacha Mungu; moyo wake ulikuwa ukiwaonea shauku. Naye akaangalia ng'ambo ya Yordani. Huyu hapo kwenye Yordani: Yordani, kiroho, ndiyo ninayozungumzia. Naye huyu hapa amesimama pale, mauti ilikuwa inamkaribia. Lakini akaangalia, na hapo karibu naye ulikuwako ule Mwamba. Yeye aliukanyaga tu huo Mwamba, nao Malaika wakaja, wakamchukua.

95 "Sitakuacha kamwe wala sitakupungukia." Haijalishi nyakati zinakuwa ni ngumu jinsi gani, jinsi gani tunazeeka, ni kifo cha aina gani tunachokufa, kumbukeni, Mwamba huo utakuwako pale Yordani. Hautatuacha kamwe wala kutupungukia. Kumbuka tu jambo hilo. Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani utakuwa pamoja nasi kote katika maisha, na hata kwenye Yordani.

96 Hebu na tuinamishe vichwa vyetu. [Unabii umetolewa — Mh.]

Wakati huyo Roho anapotembea miongoni mwetu, Roho wa Mungu akitembea miongoni mwetu, je! kungekuwako na wale hapa asubuhi ya leo wasiomjua Kristo, na wewe—wewe hujaukaribia huo Mwamba, hamko katika hali ya kuzungumza Nao asubuhi ya leo? Lakini unajua Upo. Uangalie ukitenda kazi kila mahali, mwone Yeye akizunguka kila mahali, uuone ukitembea juu ya watu. Huo ni Uwepo udumuo wa hayo Maji. Huo ni wokovu. Huyu Ndiye Roho anayevijaza vikombe vyao kufikia mahali ambapo wasingeweza kutulia tena, kitu fulani hakina budi kutokea. Wala humjui, ungetaka kuinua mkono wako na kusema, "Niombee, Ndugu Branham. Sasa ninataka kumjua Yeye. Nami ninataka kuzungumza Naye, nami ninataka kumjua Yeye kama utimilifu wa Roho Wake. Ninataka kujua ya kwamba Yeye yuko pembeni yangu daima, wakati wote. Ninaamini Yeye yuko. Lakini ninataka kuwa katika hali ya kuzungumza. Nami nina kiu, nami nina njaa ya Mungu. Ninataka kumjua vizuri zaidi?"

97 Mungu akubariki, bwana. Na Mungu akubariki, bwana. Nawe, ndugu. Ninyi, naam, huko nyuma kabisa. Chini hapa, mama, naam. Naam, mama. Tunaona mikono yenu, na Mungu anaiona. Mungu akubariki, kijana. Mungu akubariki. Na wewe, mama. Amina. Mungu akubariki. Ubarikiwe, dada. Mtu mwingine sasa katika wakati wa kimya. Mungu akubariki, huko nyuma kabisa, ewe kijana.

Wazia jambo hilo. Liwazie, Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani, Roho yule yule; ambaye Yeye alipiga mayowe pale kwenye siku ya hukumu kwa ajili Yake, wakati alipoichukua hukumu yetu. Na fimbo ya hasira za Mungu ikampiga, nazo dhambi zako zilikuwa zimefungwa kwenye fimbo hiyo, nayo ikampiga, ndipo Damu Yake na maji yakabubujika kutoka Kwake. Yeye alisema, "Baba, mikononi Mwako naiweka Roho Yangu." Na kwenye Siku ya Pentekoste, akaja apate kuambatana nasi katika safari. Naye yuko karibu sana sasa.

98 Utaninii ...?... Kutoka chini, mbali sana na Nyumbani, useme, "Bwana, ninakuja Nyumbani." Tunapoimba huu, kama ungetaka kwenda madhabahuni na kuweka wakfu nafsi yako pia, kwa Kristo ... Amina.

Nimetangatanga mbali na Mungu, (kutoka njiani)

Sasa naja nyumbani;

Njia ya (kutokuamini ni dhambi) nimeipitia kwa muda mrefu,

Bwana, naja nyumbani.

Naja nyumbani, naja nyumbani,

Kamwe sitatangatanga tena;

Ifungue kabisa mikono Yako ya upendo,

Sasa, Bwana, naja nyumbani.

[Ndugu Branham anaendelea kuuvumisha, "Bwana, Naja Nyumbani" - Mh.]

99 Wavulana watatu wadogo ndio kwanza wajitokeze, upesi sana, machozi machoni mwao, wanapiga magoti kando ya madhabahu. Bila shaka wamesamehewa. Walisamehewa hata kabla hawajaondoka vitini

mwao, hapo maskini mioyo yao ilipofanya uamuzi. Walikuja tu mbele na kupiga magoti hapa, kuwafanya watu wajue hilo, kwamba wako upande wa nani, asubuhi hii.

Ningefikiri ya kwamba kungekuwako na watu wenye umri mkubwa zaidi wangetaka kufanya hivi, wangetaka tu kupiga magoti, na kusema, "Bwana, ni—nimezurura mbali na njia. Nimekuwa na shaka sana, na wakati mwingine nilitangatanga na kuingia katika dhambi. Na—na—nataka kurudi kabla ya kuchelewa sana. Mungu, ni—ningetaka kuja. Ningependa sana kuja na kupiga magoti." Amina.

100 Sasa, wasichana watatu wadogo wa Arthur Beam, karibu wamelingana kwa kimo, wamepanda huku, wakapiga magoti.

Anayekuja mbele ni msichana mdogo ambaye ndiyo tu amempata ndugu mdogo mpya. Hivi majuzi nililisema. Bibi Wood akaja na kuniambia, akasema huyu dada alikuwa akienda hospitalini kujifungua mtoto. Roho Mtakatifu akasema, "Nenda ukawaambie atakuwa ni mvulana." Wakati alipozaliwa, alikuwa ni mvulana mdogo.

Inaonekana ni watoto asubuhi ya leo, jamaa hawa wadogo wanaotoka kwenye darasa dogo la Dada Arnold, wakiyaweka maisha yao wakfu. Madhabahu yote, kwenye mkono wangu wa kulia, yamejaa watoto wadogo.

101 Lingekuwa ni jambo jema kama tungeimba na kutoa madhabahu kwa watu wengine walio watu wazima.

Sasa, Bwana, naja nyumbani.
Naja nyumbani ...?...
Kamwe sitangatanga tena;
Ifungueni kabisa mikono Yako ya upendo,
Sasa, Bwana, naja nyumbani.

102 Na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi, kwa ajili ya jamaa hawa wadogo.

Baba wa Mbinguni, kama kukiwapo na kesho inayokuja, kama Yesu atakawia kwa miaka mingine kumi ama kumi na mitano, hawa watakuwa ndio wavulana na wasichana ambao wataupeleka huu Ujumbe kwa vizazi vingine vijavyo. Sina shaka moyoni mwangu, Bwana, ila kwamba siku zote za maisha yao watakumbuka wakija kwenye haya madhabahu. Nao ni vito vidogo, Bwana. Mioyo yao michanga na ya kitoto imehukumiwa asubuhi ya leo. Hata hawajausikia Ujumbe wote; ndio tu watoke mle chumbani, wakitoka kumsikia Dada yetu Arnold akinena; wakaja kuyazunguka madhabahu hapa, wakiyatoa maisha yao madogo Kwako.

Sasa, Baba, ndiyo kwanza nimalize kuzungumza ya kwamba ndani yetu mnakaa Roho Mtakatifu. Na huyu Roho Mtakatifu, imani pamoja na Roho huyu, hufanya mambo yote. Nami ninaamini ya kwamba saa hii hasa, unasamehe kila dhambi waliyotenda. Nami ninakuomba Wewe, kwa imani yote iliyo moyoni mwangu, ya kwamba utayadumisha maskini maisha yao kote safarini. Jalia kamwe wasitangatange kutoka kwa Njia hiyo.

103 Hili kweli ni jambo geni. Roho alisema asubuhi ya leo tungeona kitu cha ajabu. Mungu, kama umeacha kuwashughulikia hao wengine, wachukue watoto wadogo. Jinsi ambavyo asubuhi ya leo, kwenye wito wa madhabahuni, hakuna hata mtu mzima mmoja, bali kundi zima la watoto wadogo limekuja huku. Hata hivyo, ulikuwa ni Ujumbe mkuu ulio mgumu kueleweka, hata kwa watu wazima, bali watoto hawa walishika Roho Yake. Tunakushukuru kwa ajili yao, Baba. Ninawakabidhi Kwako, kama mtumishi Wako, kama tunu za mkutano huu; kwa, tukikumbuka ya kwamba Uwepo udumuo wa Maji ya Uzima utabubujika pamoja nao mradi wangali hai. Jalia wapate imani sasa katika yale yanayotendeka, kwamba Mungu aliyewavuta kutoka kitini na kuwatuma huku juu, jalia wawe na imani katika huyo Mungu siku zote za maisha yao. Jalia maskini roho zao ziletwe Kwako katika siku ya kufa kwao; zirudishwe kwenye mwili wao kwenye siku ya ufufuo. Wao ni Wako, Baba. Tunawakabidhi Kwako kwa Jina la Yesu.

104 Huku tumeinamisha vichwa vyetu. Nitawauliza watoto hawa wote madhabahuni, wanaoamini ya kwamba Yesu ni Mwokozi wako na Ndiye aliyekwambia, huko nyuma katika wasikilizaji, uje hapa na kupiga magoti kuyazunguka haya madhabahu. Je! Unaamini ya kwamba Yesu anakupenda na anakusamehe dhambi yako? Ninawatakeni ninyi nyote msimame kwa miguu yenu na kuangalia nyuma kuelekea wasikilizaji. Ninii tu ... Hivyo ndivyo unavyoweza kuwaambia watu ya kwamba unaamini ya kwamba Yesu anakuokoa. Sasa, simama kwa miguu yako, hiyo ni kweli, na uangalie moja kwa moja nyuma kwa wasikilizaji. Ninyi nyote wavulana wadogo na wasichana mnaompenda Yesu, simameni na kuangalia nyuma kwenye kusanyiko pale, kila mmoja wenu.

105 Vipi kuhusu ninyi wasichana wadogo hapa mbele? Mnaamini? Unampenda Yesu? Hawa wasichana wadogo hapa, mnapenda Yesu kwa moyo wenu wote? Mnapenda? Mnapenda? Unampenda, mpenzi? Simama hapa juu, hebu watu wajue ya kwamba unampenda Yesu. Mungu akubariki.

Sasa hebu tugeuke upande huu na tuwaimbie watu hawa kabla hatujaondoka, "Yesu anipenda! hili najua. Biblia inaniambia hivyo. Mnaona? Hebu na tuinue tu mikono yetu tunapouimba sasa. Vema, hebu tuuimbe.

Yesu ananipenda! hili najua,
Kwa kuwa Biblia inaniambia hivyo;
Watoto wadogo ni Wake,
Wao ni wanyonge ...

Sasa ...?... Watoto sasa, huku mmeinua mikono yenu, wote wakiimba, wote kwa pamoja.

Naam, Yesu ananipenda,
Naam, Yesu ananipenda,
Naam, Yesu ananipenda,
Biblia inaniambia hivyo.

106 Sasa ninyi nyote fuatisheni nyuma yangu. Ninaamini [Watoto madhabahuni wanasema, "Ninaamini"—Mh.] Yesu Kristo ["Yesu Kristo"] ni Mwana wa Mungu ["ni Mwana wa Mungu."]. Leo ["Leo"] Ninamkubali kama Mwokozi wangu binafsi ["Ninamkubali kama Mwokozi wangu binafsi."]. Tangu leo, ["Tangu leo,"] tangu sasa, ["tangu sasa,"] nitampenda ["Nitampenda"] na kumtumikia. ["na kumtumikia."] Amina. ["Amina."]

107 [Ndugu fulani katika kusanyiko anasema, "Ndugu Branham, nina watoto wanne moyoni mwangu wakati huu. Tafadhali waweza kuwaombea?" - Mh.] Hakika nitafanya hivyo, Ndugu Ben.

Baba wa Mbinguni, mtu huyu anawaona hao watoto wengine wadogo wakimjia Kristo, naye analia, kama baba, kwa ajili ya watoto wake wadogo. Na Roho aliyewaleta watoto hawa madhabahuni, jalia Roho yeye yule awaokoe watoto wake, Bwana. Tujalie. Tunawakabidhi Kwako, Baba, katika Jina la Yesu Kristo.

108 Sasa, wakati ninyi watoto wadogo mnaporudi kitini mwenu, ninataka kila mtu kwenye safu hiyo apeane mikono na watoto hawa wadogo, ama kuwapongeza wanaporudi. Rudini kwenye viti vyenu upande huu. Na hebu kila mtu pale awapongeze jamaa hao wadogo. Nasi tunawapenda kwa mioyo yetu yote. Ninyi ni washiriki wa Mwili wa Kristo, mko tu ndani Yake kama wengine wetu.

Tunatembea kuelekea Sayuni,
Sayuni nzuri, nzuri;
Tunatembea kuelekea Sayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.
Njoni, sisi tumpendao Bwana,
Na acheni furaha zetu zijulikane,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi,
Na hivyo mkizunguke ...

Huo ni uimbaji mzuri sana! Hebu na tuinue mikono yetu juu sasa.

Tunatembea kuelekea Sayuni,
Sayuni nzuri, nzuri;
Tunatembea kuelekea Sayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

Hebu na tupeane mikono sisi kwa sisi tunapoimba sasa.

Tunatembea kuelekea Sayuni,
Sayuni nzuri, nzuri;
Tunatembea kuelekea Sayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

109 Sasa, hebu tusimame huku tumeinamisha vichwa vyetu tunapoomba. Ndugu Teddy, ninii tu ... [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Twaenda Sayuni* — Mh.]

Nina haja fulani hapa, na lesa na kadhalika. Huenda zimekuja kutoka nchi za ng'ambo. Billy alikuwa akiniambia walikuwa na jozi ndogo ya vijibuti kutoka kwa maskini mtoto mchanga huko Uingereza, urefu kama huu, maskini kijitoto hicho kimelemaa kabisa. Na kwa hiyo tulikuwa tumwombee huyo, pia.

110 Na kwa hiyo ... Katika kusanyiko, Ndugu Ben anasema, "Ndugu Branham, samahani kwa kuingilia, bali omba ya kwamba, yule aliyeligonga gari letu jana usiku, kwenye bamba langu la mkono wa kulia, omba ya kwamba hiyo itafunuliwa. Omba kwamba Bwana afunue jambo hilo." - Mh.] Amina, Ndugu Ben, hakika nitafanya hivyo.

[Ndugu Branham anaendelea kuvumisha, *Twaenda Sayuni* — Mh.]

111 Tunapotembea kwa utaratibu, Bwana, tunajua ya kwamba Mwamba uliopigwa uko moja kwa moja pamoja nasi, Uwepo udumuo wa Maji yatokayo Mwambani unaambatana na Kanisa. Ee Mungu wa Milele, tufungulie asubuhi hii imani katika Mungu huyu aliye pamoja nasi. Ninajua utafanya hivyo, kama tu tunavyoweza kupata kibali Kwako, ya kwamba unaweza kutuamini. Kama ukitupa Hiyo kwa wingi, huenda tukaitumia vibaya, Bwana. Lakini kama tukipata neema Kwako, hebu na itendeke.

Ndugu yetu alisema mtu fulani aligonga gari lake. Ee Mungu, tunajua mtu huyo hana pesa za kufanya mambo haya. Ninaomba ya kwamba utamfanya mtu huyo ajihisi ana hatia, ama chochote kile, aweze kutubu kwa kufanya jambo hili, aje, aseme, "Ndugu, nitalitengeneza gari lako, nililigonga." Msaidie Ndugu Ben na wapendwa wake.

112 Hizi hapa zilizowekwa mkononi mwangu ni lesu na haja, tuna imani katika huyo Mungu. Musa alikuwa na imani katika Mungu huyo naye akavuka bahari. Danieli alikuwa na imani katika Mungu huyo, na akatolewa kwenye tundu la simba. Shadraka, Meshaki, na Abednego walikuwa na imani katika Yeye, nao wakauzima ule moto. Paulo alikuwa na imani katika Yeye, ndipo siku moja wakati ibada zilipokuwa ngumu sana naye Paulo asingeweza kumfikia kila mtu, yeye alichukua tu lesu, akasema, "Ninaamini ya kwamba Mungu yu pamoja nami." Aliweka mikono yake juu ya lesu na vitambaa, na roho za uovu zikawaacha watu, na magonjwa na magonjwa yakawaacha. Mungu, nina imani katika Mungu yule yule. Jalia uovu uondoke. Maradhi, magonjwa, mateso, jalia yaondoke, Bwana.

113 Wewe Ndiwe Mungu yeye yule aliyenena nami huko chini kwenye ile Nguzo ya Moto, huko chini mtoni. Wewe Ndiye uliye na picha Yako ikining'inia hapa pamoja nami, ukutani. Wewe uko pamoja nasi, Bwana. Wewe upo daima, Nguzo ile ile ya Moto. Nasi tumefurahia Maji kutoka kwenye Mwamba kila siku, tunaposhangilia katika Roho. Ndipo uko hapa. Tuna imani Kwako, Bwana. Tuna imani Kwako. Tunaamini ya kwamba utatutia mafuta na kutusaidia. Si kwa ajili ya utukufu wetu, Bwana; tungekuwa kama Musa wakati huo, wakati alipofanya jambo baya. Tunataka kufanya jambo fulani kukusaidia Wewe, Bwana. Hilo ndilo kusudi la moyo wetu, kukusaidia Wewe, kama tunaweza kufanya jambo hilo. Wewe tuoneshe, Baba, lolote unalotutaka tufanye.

114 Na sasa, juu ya tendo la imani, ninayahukumu maradhi ambayo lesu hizi zinayawakilisha, na haja hizi. Yatawaondokea watu hawa. Ninajua utafanya hivyo, Bwana. Ninaamini jambo hilo moyoni mwangu, ya kwamba utafanya hivyo. Ponya magonjwa yote miongoni mwetu asubuhi ya leo.

Waokoe wale walioinua mikono yao, waliosema wangetaka kuja kwenye Mwamba kwa ajili ya Maji. Mungu, hebu waone kiu sana leo, jalia kuwe na maisha yaliyokolea chumvi kwao, mpaka itawafanya kumwonea Kristo kiu. Tujalie.

Uwe pamoja nasi usiku wa leo, Baba. Ee Mungu, hebu nione, kupitia maombi haya, yaliyo mioyoni mwa watu. Kama hamna kitu moyoni mwao, basi, Bwana, nipe kitu cha kuhubiria mioyo yao usiku wa leo.

115 Mbariki Ndugu yetu Neville, na mkewe, familia yake; kanisa letu dogo, wadhamini wetu, mashemasi wetu, washiriki wetu, na Mwili Wako kila mahali; uwe pamoja nasi, Baba. Tunakabidhi jambo hili mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo.

Sayuni; tunatembea kuelekea Sayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.

Sasa, hebu tuuimbe tu, vizuri, vizuri sana Kwake sasa. Mnaona?

Njoni, sisi tumpendao Bwana,
Na tuache furaha zetu zijulikane,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Jiungeni na wimbo kwa uwiano mtamu,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi,
Na hivyo mkizunguke kiti cha enzi.

Pamoja na mioyo yetu iliyoinamishwa sasa.

Tunatembea kuelekea Sayuni,
Sayuni nzuri, nzuri;
Tunatembea kuelekea Sayuni,
Ule Mji mzuri wa Mungu.



www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7